

NI MIMI



Asante, bwana.

² Habari za jioni, marafiki. Mnaweza kuketi. Bila shaka tunayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa, usiku wa leo, katika ibada ya Kristo. Tunataka kuwashukuru ninyi nyote watu wazuri hapa katika Grande Prairie kwa ajili ya wakati huu mzuri wa ushirika, kamwe hatutausahau. Nikitumaini kwamba kama ni mapenzi ya Mungu kwamba ningeweza kurudi tena wakati mwingine nipate kuwa pamoja nanyi, labda nikae muda mrefu zaidi. Kwa njia tu isiyoweza kutegemewa ambapo ndugu yetu alipata habari nao wakajitayarisha, upesi sana, kwa ajili ya kuja kwetu. Hakuwa na wakati wa kukutangaza.

³ Nami mara nyingi nimekuwa fidhuli kuwachelewesha ninyi wananchi wakulima usiku sana, tukijua majira yenu ya kulima na kadhalika yamewadia sasa. Kwa hiyo ninasikitika kwamba niliwachelewesha, lakini natumaini ya kwamba jambo fulani lilisemwa ama kufanywa ambalo litadumu kote katika Umilele kwa ajili yenu.

⁴ Bila shaka ninataka kumshukuru huyu mchungaji, wachungaji hawa wote wazuri, wanaoshirikiana hapa ambao walikuja. Nina furaha sana kwamba ninyi watu mna wachungaji kama hawa, ambao wanalichunga kundi la Kristo. Sasa, nikitumaini ya kwamba huu mkutano, matokeo yatadumu kwa muda mrefu kwenu, kwamba kamwe hamtasahau huku kuzuriwa na Bwana wetu.

⁵ Nilisikitika kuwajia nimechoka sana na kudhoofika, lakini kama mjuavyo, nilikuwa nikipanda kwenda kuwa na muda kidogo wa kuvua samaki na kuwinda pamoja na marafiki fulani huko kwenye Kijito cha Dawson. Nami hivi punde nimekuwa niwe uwanjani kwa miezi sita mfulululizo, kwa hiyo nimechoka sana. Mikutano haijaninii, haiko jinsi ilivyopaswa kuwa, kwa sababu ono la kwanza ama mawili, basi nimekwisha tu. Na mtu yeyote anajua ya kwamba katika mikutano ya kawaida wakati mwingine kuna thelathini ama arobaini katika usiku mmoja. Na kwa hiyo, ni—ni kwa sababu nimekuwa mchovu sana, si kwa sababu ya imani yenu.

⁶ Jambo lingine, nafikiri kama tulikuwa na ibada ya mafundisho kuwajulisha watu, wengi wao, ni mapya kwao. Wakati Roho Mtakatifu... Unapoomba, wewe kuwa ukiomba na kukumbuka ya kwamba Mungu anajiandaa kujibu maombi yako papo hapo. Na mara anaponena, wewe simama, hiyo ni kusema, upesi, hiyo ni kusema, Mungu anakutaka ufanye haraka, unaona, na kulisimamia.

7 Mnaona, mara nyingi, ningeona ono juu ya mtu fulani kisha ningezungumza na—na kama hawaitikii, linaenda moja kwa moja kwa mtu mwingine, mnaona, na halafu, ni mwoga sana, Roho Mtakatifu ni mwoga sana. Naye ataondoka. . . Labda mtu huyo ameketi pale kwa nia njema, akiamini, hilo lingewasaidia kidogo. Halitawaponya, haliwaponyi, lakini li—linawapa ujasiri kujua ya kwamba maombi yao yalimgusa Kuhani Mkuu. Na wakati mwingine kwa njia hiyo wa—wanaukosa kwa kutojua jinsi ya kuishikilia, ni kitu kipya.

8 Na si zaidi ya vile mchungaji wenu, mtu mwingine yeyote anayewaombea, kwa sababu hata hivyo, ni maombi tu ya imani ndiye yanayomwokoza mgonjwa huyo. Mchungaji ana haki tu ya kukuombea kama mtu yeyote aliyeko. Na kama mchungaji wako hayupo, mtu mzuri, mtakatifu katika ujirani, mtu yeyote, maana, “Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, ili. . .” Maandiko, ninaamini, Yakobo Mtakatifu mlango wa 5.

9 Na imekuwa ni ajabu sana. Mara nyingi nashangaa wakati mwingine jinsi ambavyo mambo mengi sana hutendeka, bali ni maombi rahisi tu. Ninapanda juu na kumwombea mtu fulani, labda yuafa, kansa ya sarkoma ama kitu fulani, ameliwa tu, baada ya kitambo akienda zake, “Unanikumbuka, Ndugu Branham? Mimi ndiye niliyekuwa *hivi-na-hivi*,” makumi ya maelfu yao, kote ulimwenguni.

10 Kwa hiyo, mnaona, ni imani rahisi tu, si kitu, si chochote tunachojisukumia, ni kitu tu tunachoamini kama vile mtoto angeamini, kama tu vile ungemwahidi msichana wako mdogo nguo mpya Jumamosi, huyo mvulana mdogo koti la ovaroli. Unaona, wanatarajia jambo hilo. Imani rahisi tu kama ya kitoto, hivyo tu ndivyo Mungu anavyotutaka tuwe, kwa sababu sisi ni watoto tu kwa vyovyote vile.

Na kwa hiyo tu—tuna furaha kuwa na wakati huu wa ushirika pamoja nanyi. Mungu na awabariki, pia.

11 Ninashukuru sana kuona kanisa hili jipa, dogo, la kupendeza. Inaonyesha kuna kusanyiko linalostawi ambalo lingejitolea kujenga kanisa kama hili katika hii. . .mji huu mdogo hapa, na idadi yake ya watu inayoongezeka. Ninatumaini ya kwamba Mungu atalipanua hata itawabidi kununua ploti jirani na kujenga jengo kubwa zaidi, na mamia mengi ya watu wakiokoka.

12 Mungu ambariki mchungaji, na mashemasi, na wadhamini, na washiriki wengine wote walio pamoja nasi hapa. Hatujagawanyika, sisi ni Mwili mmoja. Tunaamini ya kwamba kuna Kristo mmoja aliyetuokoa sisi sote. Na kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyosimama.

13 Na sasa, labda hivi karibuni nitakuwa katika nchi za kigeni tena. Na sasa, hapa Marekani unaweza tu kutoka nje, uhubiri,

na labda kuweka mikono juu ya wagonjwa, hilo ni sawa, upite nayo. Lakini si wakati ukiwa kwenye mstari wa mbele wa vita. Huko nje u—unakabiliana na pepo, ni—ninamaanisha kuwapa pepo changamoto, wachawi na, loo, kile wanachoita, “watu watakatifu,” na—na kila kitu, ambao hawaogopi kutoa changamoto. Lakini nasema hivi, Mungu akiwa ni Hakimu wangu, sijawahi kuona moja likitukia pasipo Mungu kushinda kwa ushindi mkuu, namna hiyo, kila wakati, kila wakati.

¹⁴ Tuna vitabu, ila sikuwazia kuvileta. Kama ungetaka kimoja, ama chochote kile, tuandikie tu huko Indiana, Jeffersonville, Indiana, tutafurahia kukituma. Na kama wakati wowote unahitaji kitambaa cha maombi na unataka kukibeba katika Biblia yako, vema, niandikieni tu, Jeffersonville, Indiana, tu. Tutakituma, bila malipo. Hakuna kulipia chochote, hatulipishi chochote, kila kitu ni bure. Yesu alisema, “Kama mliyopata bure, toeni bure.” Kwa hiyo sisi. . . Hakuna kulipia cho- . . .

¹⁵ Kweli tuna vitabu, ila si vyangu, ni vitabu ambavyo watu wengine wameandika kuhusu huduma hii. Kwa hiyo inatubidi kuvinunua, nasi tunapata punguzo la asilimia arobaini juu yake. Halafu inatubidi kuvikokota kuvipeleka mikutanoni, na daima tunaviweka mikutanoni na—na kumchukua mtu wa kuviuza. Tunawapa vijana kadhaa, wanaoambatana nasi, dola hamsini kwa juma kuuza vitabu mwanzoni mwa mkutano, mwishoni mwa mkutano, hatutaviuza Jumapili. Halafu tuna maagizo, haidhuru ni nani, kama huyo mtu akija na anataka kitabu naye hana pesa, wape kwa vyovyote vile. Mnaona? Wala kamwe usimnyime mtu, kwa sababu sio kuuza kitabu, sikuzote ni kueneza Ujumbe.

¹⁶ Na mtu yeyote anajua, ninyi ndugu mnaouza vitabu, hakuna pesa katika kuuza vitabu, isipokuwa uninii. . . hakuna chochote. . . hata havijilipii. Sadaka ya upendo ndiyo inayovilipia hivyo vitabu, kwa watu ambao. . .

¹⁷ Wakati mwingine ninapoondoka kwenda kwenye uamsho mkubwa, watanipa sadaka ya upendo. Basi ninapofanya hivyo, ninaipeleka kanisani mwangu, ninaikabidhi kanisa, nayo inaenda kwenye misheni za kigeni. Kutokana na hiyo wananipa pesa za kutosha kuishi: dola mia moja kwa juma kwa familia yangu, na—na nyumbani, na motokaa, na matumizi, na kupiga simu, na kadhalika. Bila shaka, hiyo haitumiki kwa zile simu zingine, mamia ya dola yanatumika kwa mwezi, kwa kupiga simu. Nami nimeona wakati ambapo simu za mbali peke yake zingekuwa na wastani wa sitini na nne kwa saa. Kwa hiyo mnaweza kuwazia ni kitu gani.

¹⁸ Si mahali pamoja tu padogo, ni kote ulimwenguni. Mnaona? Na watu wamekaa mle ndani walingojea kwa miezi kadhaa, mamia yao kwenye orodha ya wanaongojea sasa, kwa dakika chache tu, wanatoka Afrika, India, Asia, kila mahali kuja

kwenye mahojiano hayo ya faraghani. Sasa, hapo ndipo unasimama mbele za Mungu na kungojea mpaka Yeye anene na kusema kile hasa kinachopaswa kufanywa. Na hakuna hata wakati mmoja Yeye alipowahi kutupungukia. Kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo, tunamshukuru Mungu.

¹⁹ Sasa, ninapanda kwenda kwenye Kijito cha Dawson tena, nasi tunawaalika huko. Ndugu Sothmann alikuja na kunichukua muda mfupi uliopita, yeye na mwanangu, nilipokuwa chumbani nikiombea mkutano usiku wa leo, naye akasema watakuwa na kiamshakinywa, ninaamini, Jumamosi asubuhi, hiyo ni nzuri. Nasi tutafurahia mkija, kuhudhuria kiamshakinywa, kuhudhuria mkutano. Halafu nmiombe. Halafu nmiombe.

²⁰ Ninataka kuwaomba fadhili hii moja, kabla sijayafungua Maandiko. Mnajua wakati pepo motomoto zinapovuma, na kila kitu kinaenda kinyume, na wachawi kila upande, nguvu za ibilisi zikitoa changamoto kila upande, sijui kama ningeweza tu kuwategemea ninyi, huku nyuma, katika Grande Prairie wakati fulani kila siku kuniombea dua ndogo. Mtafanya hivyo? Mtaniahidi kufanya hivyo? Nawashukuru. Asanteni. Daima nitawakumbuka.

²¹ Kila wakati nikipita, ninajaribu kusimama na kuwaona ninyi, kama ninakuja na kurudi. Na kama nisipowaona tena mpaka tutakapovuka ule mto, nitawaona Ng'ambo ya pili kule, ambako... Halafu basi kumbukeni, Injili ile ile ninayofundisha habari zake usiku wa leo, nitakuwa nimesimama kule nimeishika mkononi mwangu. Nikisema, "Ilikuwa ni kweli." Nami nina hakika Bwana wetu atathibitisha hilo, kwamba ni kweli. Si kwamba tu anafanya hivyo wakati huo, bali anafanya sasa, ambapo, Yeye anafanya sasa, hiyo ni kweli.

²² Hakika ninawathamini na kuwapenda kwa upendo mchangamfu, wa Kikristo. Na kama wakati wowote ninaweza kuwafadhili, nipigieni simu ama mniandikie, nitafanya chochote niwezacho kuwasaidia, kuwarahisishia maisha, na kufanya mahali panapoparuzi kuwa laini kidogo. Wakati wowote ninapoweza kuwaombea, kuwafanyia lolote, nijulisheni.

²³ Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja, tunapozungumza na Mwandishi wa Neno hili.

²⁴ Bwana, Mungu wa uumbaji wa mbingu na nchi, aliyeumba vitu vyote kwa Kristo Bwana wetu, Yule aliyemtuma kuwa upatanisho wa dhambi zetu, akitupatia Neno Lake, ambalo ni Maji ya farakano, akatuosha kwa Maji, kwa Neno la farakano, ili kwamba kwa imani, tukiamini ya kwamba tumetengwa na dhambi zetu, tumeitwa, tukatengwa, tukakusudiwa kwa ajili ya Injili ya Bwana Yesu, "habari njema," inaenea kote kutoka mimbarani Bwana, hata kwa maskini mke wa nyumbani ambaye angeweza kushuhudia na kusimulia wema wa Mwokozi wetu aliyebarikiwa, tunainamisha tu vichwa vyetu kwa unyenyekevu,

Bwana, na kukushukuru Wewe, kujua ya kwamba wakati mmoja tulikuwa tumetengwa na Mungu, bila tumaini, bila Kristo, bila Mungu, na tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa badala yetu apate kutupatanisha turudi kwenye familia kuu ya Mungu. Kwa hiyo tutaninii. . . hatungeweza Bwana, kwa hotuba ya binadamu, daima kuonyesha ibada ya mioyo yetu kwa ajili ya wema na rehema Zako kwetu. Lakini, Baba, katika njia yetu rahisi, nyenyekevu, kama ya kitoto, pokea shukrani zetu, Bwana Mungu.

²⁵ Sasa, ninaomba, Baba, kwanza kwa ajili ya wahudumu Wako hapa kwenye. . . ndugu zangu. Ee Mungu, nina furaha sana kuwa na ushirika pamoja nao. Ilisema wakati mmoja katika Biblia ya kwamba “Jinsi ilivyo vema ndugu wakae pamoja kwa umoja! Ni kama mafuta yaliyokuwa kwenye ndevu za Haruni, yashukayo mpaka upindo wa vazi lake.” Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hilo, Bwana, kwa ajili ya ndugu wa imani moja ya thamani, wanaomwamini Mungu. Tunakushukuru kwa ajili ya makanisa yao. Nami naomba, Mungu, ya kwamba utabariki jitihada zao, popote walipo, na jalia haya makusanyiko yakue, na neema ya Mungu iwe pamoja nao, Bwana. Jalia ishara na maajabu yaambatane na huduma yao, Bwana, tupate kulitikisa taifa hili kwa nguvu za Mungu. Tujalie, Bwana.

²⁶ Tutumie watu kutoka kwenye nyika hii kama Yohana Mbatizaji, aliyejitokeza kwa ukakamavu na kukaripia, nabii huyo, akinena juu ya Masihi ajaye na “Pepeto Lake mkononi Mwake, ambaye angesafisha kabisa sakafu Zake, na kuyateketeza makapi kwa Moto usiozimika.”

²⁷ Sasa, Baba Mungu, bariki kusanyiko hili, usiku wa leo. Hawa hapa akina mama wameketi pamoja na watoto wao wachanga, naona kina baba na mama wameketi pamoja, na wagonjwa, na wahitaji. Ninaomba Mungu, ya kwamba Malaika wa rehema atapitia hapa, usiku wa leo.

²⁸ Jalia kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu, ibada hii itakapofungwa. Jalia twende katika makazi yetu, usiku wa leo, tukishangilia, tukisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Tujalie, Bwana, kwa kuwa tunajua Wewe unabaki yeye yule jana, leo, na hata milele.

²⁹ Wabariki watu hawa, Baba, na ikitokea kwamba baadhi yetu tutavuka mto kabla hatujaonana tena, Mungu, jalia kwamba sote tutakutana tena mahali fulani huko, katika ile ng’ambo kuu, na huko tutashirikiana pamoja milele.

³⁰ Jinsi ningetaka kwenda nyumbani pamoja na kila mmoja wa wanaume na wanawake hawa, kuyatembelea makazi yao! Ingekuwa ni baraka kwangu, Bwana, kuketi chini na kusoma Maandiko, kupiga magoti mezani pao, na kuomba. Ingekuwa ni neema jinsi gani! Lakini, Baba, kumekuchwa, jua linatua, Umilele unaingia. Loo, hatuna budi kupiga vita kadiri

tuwezavyo. Mungu, kama kamwe sitapata kufanya hivyo katika ulimwengu huu, jalia niweze kufanya hivyo katika ulimwengu ujao.

³¹ Tupe neema Yako. Jalia Roho Mtakatifu anene nasi, usiku wa leo, kupitia Neno lililoandikwa, funga vinywa vyetu kwa chochote ambacho kingekuwa kibaya, kisha ufungue mioyo yetu kabisa tupate kulipokea. Jalia Mbegu ianguke katika udongo mzuri ambao utazaa mara mia, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Tunaomba hayo, katika Jina la Mtoto Wake mpendwa, Bwana Yesu Kristo, Mwokozi wetu. Amina.

³² Ningetaka tu kurejea kwenye A—Andiko, usiku wa leo. Nami nilisikitika sana kwamba niliwachelewesha jana jioni. Nilikuwa nikizungumza na nyinyi. . . Mimi huzungumza tu kupita kiasi. Kwa hiyo mimi. . . [Ndugu mmoja anasema, “Tulilifurahia.”—Mh.] Asante, bwana. Hilo ni zuri sana, wewe, neema nyingi, Ndugu, na—nakushukuru kwa hilo, hilo ni zuri sana, linanifanya nijisikie vizuri, kujua ya kwamba unajitahidi na linathaminiwa, unajua ninalomaanisha.

³³ Sasa, sababu yangu hapa ni nini? Kujaribu kuwasaidia, kujaribu kuyafanya maisha yawe rahisi kidogo kwenu. Basi ingefaa nini kwangu kuja hapa kama laghai ama mnafiki? Silipwi kuja; siombi pesa. Sijaninii. . . Sio umaarufu, ninauepuka huo. Mnaona?

³⁴ Kwa hiyo mtu anayejaribu kuwa maarufu hawezi kupatana na Mungu. Kwa hiyo si huo, ni kwa sababu moyoni mwangu nawapenda. Nimechoka na kudhoofika, ninajiandaa kwenda kupumzika kidogo kwa juma moja ama mawili, kabla sijaingia hudumani tena. Lakini upendo wangu ulikuwa kwamba nisingeweza kuwapita bila kusimama humu, nikisema, “Mu hali gani?” na kuwa na mkutano kidogo, na kushirikiana nanyi kwa muda kidogo.

³⁵ Kwa hiyo kumbukeni, kile ninachowaambia ni hiki, ya kwamba Bwana wenu na Bwana wangu hajafa, Amefufuka katika wafu, Naye yuko pamoja nasi. Yeye. . . Sisi ni watoto Wake.

³⁶ Sasa, katika uponyaji kama utaitumia tu imani na kusema, “Sasa, kama Yeye yupo hapa, basi mtazamo Wake kwa mtu mmoja ni mtazamo Wake kwa wote.”

³⁷ Sasa, labda mtu fulani atakuwa na imani kidogo tu ya juu, ambayo itaninii, inaweza kupita yenu na kungusa Yeye, na kuleta o—ono juu yao. Hiyo haimaanishi kwamba mtu huyo ndiye pekee anayeweza kuponywa. La. Una. . . Mtazamo wa Mungu ni vivyo hivyo kwako.

³⁸ Lakini kamwe huwezi kulivumilia, linakurarua tu vipande-vipande. Ni wangapi wanaelewa hilo? Inua tu mkono wako. Yesu alisema (Samahani.), Yesu alisema, wakati mwanamke mmoja

alipogusa vazi Lake, Yeye alisema, “Naona kwamba nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka.”

³⁹ Kwa hiyo mnaweza kutambua, sikiliza ndugu yangu, dada, huenda ikawa ndio wakati wetu wa mwisho kukutana, hakuna mtu, hakuna mtu katika ulimwengu huu atakayejua yale nimepitia, hiyo ni kweli, huwezi kulielezea, huwezi kumwelezea Mungu. Nanyi mnaketi mkutanoni, si hapa ndani, lakini mara nyingi unazungumza kwa dakika chache kuona, hawa *hapa* wakosoaji *hapa*, huyu *hapa* mwenye shaka, huyu *hapa* mmoja wa kishirikina, huyu *hapa* mmoja, ambaye—ambaye *amepagawa na pepo* ameketi hapo, na hayo yote, unahisi hayo yakija dhidi yako kama pumzi.

⁴⁰ Halafu basi unaninii, unaona, kuna mtakatifu mtauwa aliyeketi *hapo* akijaribu kumtafuta Mungu, huyu *hapa* mwingine anashangaa na kutilia shaka, huyu *hapa* mtoto mchanga, yuafa, huyu *hapa* mwenye makengeza, huyu *hapa* baba ameketi hapa akiwa na kansa. Mungu akitenda. . . Na halafu hayo yote kwa maelfu, yakikukabili kwa wakati mmoja. Hamtambui jinsi linavyokuraru vipande-vipande. Mnaona?

⁴¹ Na hapo, basi wazienu tu, Shetani anangojea neno moja dogo, lilipotoka, mahali fulani. Hivyo tu. Mnaona? Na ukijua ya kwamba wewe ni mwanadamu, inakubidi kumtegemea kabisa Yesu Kristo, utupe tu maisha yako Kwake kabisa.

⁴² Sasa, katika Maandiko ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 14, na kifungu cha 27, tunasoma hivi:

Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msiogope.

⁴³ Ningependa kuchukua hilo kama somo: *Ni Mimi. Ni Mimi*, maneno matatu [Kiingereza: It Is I—Mfa.].

⁴⁴ Na sasa, nataka sisi, usiku wa leo, ili tuweze kuharakisha, kuhudhuria mkutano wa ushuhuda. Mnapenda shuhuda? Sote tunazipenda. Na si mngalipenda kuishi katika siku za mitume, na kuketi chini mahali fulani kwenye gogo kando ya ziwa, na kuwasikia hao mitume wakishuhudia? Ni wangapi wangelipenda kusikia hayo? Kuwasikia tu pamoja, wale waliotembea pamoja na Yesu!

⁴⁵ Na hakika kama walitembea pamoja Naye na kumjua Yeye, wangejua jinsi ya kushuhudia juu Yake. Hivi hamwamini hilo? Hakika. Wangejua jinsi gani. Maisha Yake, walijua kile tu alichokuwa. Basi kumbukeni, wao hawakuwa Malaika sasa, walikuwa ni watu waliokuwa na heri na shari zao, kama tu tulivyo nazo sisi.

⁴⁶ Mara nyingi watu hufikiri wakati huduma inapokuwa ya kimbinguni, wanafikiri mtu huyo anapaswa kuvaa nguo za majoho, na—na, “Usiniguse,” na mnajua. Mtu anapofanya hivyo,

wanajaribu kuwa kitu wasicho. Mungu huwatumia wanadamu, watu wa kawaida tu.

⁴⁷ Unapomwona mtu kama huyo, kwangu mimi ni mwenye kiburi, mnaona, mtu anayejaribu kuwa kitu wa—wasicho, “Mtakatifu kuliko ulivyo wewe, usiniguse. Mimi . . .” Huyo, loo, Mungu hawezi kumtumia huyo, mnajua hilo.

⁴⁸ Kwa hiyo sisi ni . . . Mungu . . . Nitasema jambo hili moja: Baadhi ya wenye mioyo mizuri sana niliowahi kupeana mkono nao, chini yake, inayopiga chini ya shati kuukuu la samawati lenye viraka, hiyo ni kweli, macho mawili halisi ya kijivu, yanakuangalia usoni na kusema, “Mhubiri, ninaamini hilo.” Ndugu, unaweza kutegemea hilo, liandike. Makovu kutoka kwenye vipini vya plau ama chochote kile, hiyo ni kweli. Haikubidi kuvaa koti rasmi, ukosi wako umepinduliwa, upate kuwa Mkristo anayemcha Kristo, la. Si kile unachovaa, ni kile ulicho ndani, ndicho kinachokufanya; si jinsi ulivyo nadhifu bali *jinsi* ulivyo kwa ndani. Kwetu sisi hakuna mmoja wetu aliye mwema, iwapo kuna wema wowote kwetu, “Kuna Mmoja tu aliye mwema na huyo ni Mungu,” Kristo alisema.

⁴⁹ Lakini ningetaka kwenda kwenye mkutano wa ushuhuda, na kuketi tu chini na kujichukulia kiti na kuwasikia mitume wakishuhudia. Loo, daima nimewazia ningependa kufanya hivyo. Sasa, daima niliwazia ningetaka kumsikia Yesu aliposema, alipoinyosha mikono Yake ya upendo na kusema, “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.”

⁵⁰ Loo, mnajua wamefikia ambapo, wanadai, kama sauti imewahi kunena, mnajua kuliko nijuavyo mimi, sauti, haifi kamwe, inaendelea kuishi, kama radiamu, inaendelea, na kuendelea, na kuendelea, kama changarawe ikianguka majini, hayo mawimbi madogo yanazidi kwenda na kwenda kwa maili kadhaa, mitetemo mpaka huwezi kuiona kwa jicho lako la kawaida, bali yanazidi kuendelea na kuendelea na kuendelea. Na hewa yako, unapozungumza, hapo ndipo unapoinyosha kwenye elektroniki na re—redio hilo wimbi la hewa, linaendelea, halifi kamwe.

⁵¹ Ningetaka, wazo, ningetaka kuishi mpaka sayansi labda ingeweza kuinasa ile Sauti Yake. Wanadai ya kwamba siku moja, kama wakiendelea kusonga mbele, wataweza kufanya hivyo, kuinasa Sauti Yake halisi, aliposema, “Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nitawapumzisha.”

⁵² Vema, huenda nisiishi hadi siku hiyo, kwa kweli, sidhani ulimwengu utadumu kwa muda mrefu hivyo, tumekaribia sana wakati wa mwisho. Lakini ningependa kuwa pamoja nanyi kuwahubiria kwa muda juu ya mambo hayo. Lakini nimejaribu

kufanya jumbe zetu ndogo rahisi tu katika mchezo wa kuigiza, maana nimechoka, na ndipo mngelielewa vizuri zaidi.

⁵³ Lakini, huenda nisiishi kusikia hayo, lakini kuna jambo moja ninalotaka kusikia na ninaamini nitalisikia, “Ulifanya vema, mtumishi Wangu mwema na mwaminifu, ingia katika furaha za Bwana.” Hilo ndilo ninalotarajia kusikia siku moja, nina hakika Yeye hatanisikitisha.

⁵⁴ Na kama mimi . . . Kama akinikataa mwishoni mwa safari, ningali nitampenda. Kama akinipeleka kuzimuni, nami ningali ninaweza kuwa na upendo kuzimuni, nitampenda kwa vyovyote vile. Mnaona? Kwa sababu nilistahili kukataliwa hapo mwanzo, mnaona. Na kama ningelikuwa na maisha elfu kumi ya kuishi, wala hakuna kitu baada ya mwisho wa hayo, kama kulikuwako—kama hakukuwako na Mungu, hakuna Kristo, bado ningechukua njia hii ya Kikristo kuishi, kwa vyovyote vile. Kuwa na wanaume na wanawake ninaoweza kushirikiana nao, inafanya maisha kuwa tofauti sana, mnaona, kama ukiwa tu Mkristo.

⁵⁵ Sasa, hebu na tuuingilie mkutano huu wa ushuhuda na kuwasikiliza mitume wakishuhudia.

⁵⁶ Hapana shaka ilikuwa yapata machweo, yapata wakati huu ji—jioni, wakati yule mvuvi mkubwa mwenye misuli migumu mgongoni alipoanza kusukuma mtumbwi kutoka ufukoni. Nami ninaweza tu kumwona anapoichukua ile meli ndogo, na mgongo wake mkubwa, wenye misuli migumu, akisukuma, akiisukuma hiyo mashua, na inapotoka ufukoni, anaisukuma majini, ikaingia katika Galilaya samawati, kisha anapanda juu kwenye viti na kuchukua mahali pake karibu na ndugu yake, Andrea. Ndipo hayo makasia madogo yakaanza kutumbukia majini, nao wangeyatumbukiza, kisha wanawaaga, “Kwaherini,” wale walio ufukoni, kwa sababu walikuwa na mkutano mkubwa alasiri hiyo, na—naye . . . walikuwa wakiondoka, nao hao watu waliwapenda.

⁵⁷ Kuna jambo fulani kuhusu upendo wa Mungu mioyoni mwetu, ambapo inatuua tu kutengana sisi kwa sisi. Kundi halisi la Kikristo wanapokusanyika pamoja, wakati inapowabidi kuachana kanisani, ni—nimewaona wakisimama tu na kukumbatiana na kulia. Mnaona? Ninawazia juu ya Paulo akipiga magoti ufukoni na kuomba, asema, “Na—na—najua hamtaniona uso tena.” Na jinsi ilivyo kutengana mmoja kwa mwingine!

Tulikuwa tukiimba wimbo huko chini katika kanisa la kale la Kibaptisti, huko kusini:

Kibarikiwe kifungayo
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja,
Ni kama wa huko Juu.
Tunapoachana,

Inatupa maumivu ya ndani;
Lakini bado tutaungana moyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

⁵⁸ Hapana shaka ilikuwa ni hisi hiyo wakati meli hiyo ndogo ilipokuwa ikiingia majini. Nao, wakiwaaga, na wote wakisema, “Rudini. Iweni pamoja nasi tena, ndugu.” Kuwaona hao watu ufukoni, nao wakiyapangusa machozi machoni mwao, na kuwapungia, “Rudini mwe pamoja nasi tena,” wakati meli hiyo ndogo ikiingia majini.

⁵⁹ Na baada ya kitambo kidogo ikatoweka. Hawangeweza kuona tena, giza lilikuwa likitanda. Nao wangekuwa, wamekuwa wakivuta. . . Katika siku hizo walivuta kwa makasia, watu wawili kwenye kiti kimoja. Nao wangechukua makasia haya na kudumisha wakati walipokuwa wakivuta hizo mashua ndogo. Ndipo basi kama upepo ulikuwa ukivuma, wanapandisha tanga dogo, na—na kuwasaidia kwenda mbele.

⁶⁰ Nao walikuwa wakivuka Galilaya. Na baada ya kupata. . . kwa kipindi kidogo cha mapumziko, tutaamini ya kwamba hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana, alikuwa ndiye mdogo kuliko wote miongoni mwao na—na hasa maskini mtume mwenye shauku kubwa. Na kwa hiyo walipovuta makasia yao kutoka majini, na hapana shaka mtu fulani alisema, “Ndugu, hebu na tu—tupumzike kidogo na tustarehe dakika chache, na tufanye mkutano mdogo wa ushuhuda.” Na huo ndio tunaotaka kuingilia.

⁶¹ Kijana Yohana hapana shaka alisema, “Vema, leo imekuwa ndiyo siku iliyolitatu kwangu milele. Nimekuwa mwaminio tangu nilipokuwa mtoto mchanga. Ninaweza kukumbuka juu ya maskini mama yangu wa thamani akinisomea hadithi za Biblia, na jinsi alivyoniambia ya kwamba wakati watu wetu walipovuka kutoka nchi za Misri, walipoletwa kwenye nchi hii tuliyorithishwa na Mungu. Alikuwa akinisimulia hadithi za jinsi Yehova alivyokuwa mkuu, na jinsi alivyowajali watu Wake.

⁶² “Na jinsi nilivyokuwa nikilala na kuutazama uso wake mrembo, naye angeniambia, ‘Yohana, kote ng’ambo ya nyota kule, kuna Mungu mkuu anayewapenda watu Wake. Usilisahau, mwanangu.’ Ndipo akaniambia ya kwamba wakati Mungu, Yehova, alipokuwa amewaita watoto Wake kutoka Misri, kwamba Yeye huwakimu wale wanaopiga hatua kutembea katika amri Zake, nao walikuwa wakimfuata Yehova kutoka Misri, nao wakatoka wakaingia jangwani kisha wakaishiwa na mikate, hawakuwa na mikate ya kula, ndipo Yehova akashusha mikate kutoka mbinguni na kuiweka juu ya nchi. Basi kesho yake asubuhi kitu pekee walichokuwa nacho, cha kufanya, ni kwenda kuokota na kuila hiyo mikate.

⁶³ “Nami nilikuwa nikimwambia mama yangu,” huenda alisema, “‘Mama, labda, Mungu ana matanuru *makubwa*

sana huko juu Mbinguni, na Malaika wengi sana wanaofanya kazi ya ziada, nao wangeoka mikate hii yote, na ndipo hao Malaika wangechukua vikapu vikubwa, na kushuka chini, na kuvitandaza kote kambini.’

64 “Akasema, ‘La, Mwanangu. Wewe ni mdogo sana kuelewa, lakini unaona, Mwanangu, Yehova ni Muumba, aliumba tu mkate huo. Haimbidi kuwa na matanuri kuuoka, Yeye aliiumba tu mikate hiyo nayo ikaanguka chini.’”

65 Na, loo, huenda Yohana alisema, “Hilo daima lilidumu moyoni mwangu, jinsi ambavyo hilo lingeweza, Yehova angeweza kuumba mikate na kuishusha chini duniani tayari imeokwa. Ndugu, ninataka kufanya maungamo yangu katika ushuhuda huu, usiku wa leo, hapa kwenye mtumbwi huu, kwamba ninajua ya kwamba hatumfuati nabii fulani wa uongo, hatumfuati laghai fulani. Kwa kuwa nilipomwona, leo, akichukua hiyo mikate midogo, mikate mitano na samaki wawili wadogo, na kuumeza mkate huo na kuwalisha watu elfu tano, nilijua huyo alikuwa ni Mungu.

66 “Hilo lilitosha kwangu kwa sababu Yeye alifanya kazi za Mungu. Mnakumbuka, ndugu, Yeye alituambia wakati mmoja hapo awali, ‘Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi?’ Lakini alifanya nini ndugu?”

67 Ninataka kuliuliza kusanyiko hili, “Ni—ni atomi ya namna gani aliyofungulia?” Alichukua biskuti hizo ndogo na kuvunja tano kati ya hizo na kuwalisha watu elfu tano, si kuotesha ngano na . . . Yeye hufanya yote ili . . . hakika. Lakini alipita taratibu zote za maumbile, si kwamba tu alikuza ngano kule, alikuza mikate, si mkate tu bali mkate *uliookwa*, tayari umekolezwa na uko tayari kuliwa. Huyo ni Mungu wetu.

68 Samaki, mbona Yeye aliweka kila samaki majini, lakini Yeye aliwachukua samaki hawa na kuwavunja, sio ati alimwinua tu samaki mwingine kutoka majini, bali alimvunja samaki kisha akarudi na kuchukua, kipande kingine kikakua wakati Yeye alipokuwa akimvunja huyo, samaki *aliyekaangwa*, tayari amekolezwa, amefingirishwa kwenye unga wa mahindi, na kukaangwa, tayari kwa kuliwa. Alifanyaje hilo? Ni atomi za namna gani ambazo sayansi ingesema leo kwamba Yeye aliachilia pale?

69 Nami ninaweza kumsikia Yohana akisema, “Ndugu, lilinibumbuwaza sana hata ni—nikapanda juu nyuma ya mwamba, na kuangalia, na kuona mahali Yeye alipokuwa, ningeweza kuona mahali alipokuwa akiitoa, bali alichukua tu mkate, akaushika, kisha akameza kipande chake, na kuuweka kwenye kikapu cha Andrea, kisha akaunyosha mkono tena, na kulikuwako na kipande kingine kilichokuwa tayari wakati alipokinyosha mkono Wake. Kwa hiyo hilo linanithibitishia kwamba Yeye ni Mungu, Yeye ni Yehova.

70 “Yehova tu wa Agano la Kale ndiye angeweza kuumba mkate, na hapa, kuwalisha watu wenye njaa, na hapa Yehova huyo amedhihirishwa. Nami ninajua ya kwamba Huyu ni Mwana wa Mungu, angeweza tu kuwa. Yeye anahusishwa na Mungu mahali fulani, kwa sababu Yeye alifanya mambo yale yale aliyofanya Mungu.”

71 Hapana shaka ilikuwa ni Simoni Petro, yapata wakati huo, aliyesema, “Huo ni ushuhuda mzuri, Yohana. Naweza kutoa ushuhuda wangu sasa? Mnajua, ndugu, ya kwamba nilikuwa mvuvi. Baba yangu, kabla yangu, alikuwa mvuvi. Baba yangu alikuwa mtauwa, mzee Mfarisayo. Nanyi mnakumbuka alitumia wakati mwingi sana kanisani, nasi tulivua samaki mtoni, hapa ziwani.

72 “Naye mama yangu, na jinsi ningemwona yeye na Baba wakinichukua mimi na Andrea, asubuhi moja, tulipoenda kuvua samaki, na kupiga magoti kando ya meza, na jinsi ningemwona Baba akiangalia juu na kusema, ‘Yehova, ninahitaji samaki leo nikawauze sokoni kuwalisha watoto wangu wadogo, utanisaidia kuwakamata wengi leo hii?’

73 “Jinsi ambavyo wakati tungewavua samaki na kuingia ufukoni, jinsi ambavyo mimi, na Andrea, na Baba, tungepiga magoti kando ya hiyo mashua na kumshukuru Mungu kwa ajili ya hao samaki kabla hatujawapeleka sokoni.” Loo, tunahitaji baba na mama zaidi kama hao, “Mlee mtoto katika njia impasayo.”

74 “Siku moja nakumbuka,” huenda alisema hivi, “ya kwamba tulikuwa tumepata samaki wengi sana siku hiyo, loo, samaki wengi sana. Nasi tukavuta mashua yetu ndogo ufukoni, nami nikaruka ufukoni na kuufungia ninii, huo mtumbwi, nami nilikuwa nikisaidia, kuwatia hao samaki kwenye vikapu.

75 “Basi tukiisha kuomba, ninaweza kumwona baba yangu akipiga brashi mvi kutoka usoni mwake, akanikumbatia kwa mkono wake, kisha akaniketisha juu ya mtumbwi, kasema, ‘Simoni, mvulana wangu mdogo, nimekulea upate kumtumikia Mungu, kadiri nijuavyo mimi.’ Naye akasema, ‘Simoni, mimi, kama waaminio wote wa kweli, nimeitazamia siku ambayo Masihi angekuja. Nilifikiri ningemwona katika siku zangu, lakini, Simoni, ninazeeka sasa, nazo siku zangu zimehesabiwa, hatua zangu zinapungua, mimi, labda, sitamwona. Lakini, Simoni, mwanangu, wewe ndiwe mdogo zaidi, kwa hiyo labda utamwona Masihi ambaye tumemtazamia, kwa miaka hii yote, Tumaini la Israeli.

76 “Simoni, kabla hajaja, kutakuwako na mambo mengi ambayo yameibuka kote katika nyakati na kusema wao ni Masihi na mambo haya yote. Na wakati, kufikia huo wakati, kuja Kwake, mambo ya kila namna yatatokea. Lakini, Simoni, makanisa yameenda kombo kwa hamaki nyingi, na,

ila nataka kukwambia, mwanangu, wewe kumbuka kuamini yale Musa aliyosema, manabii wetu, ya kwamba Masihi huyu ajapo, Musa alitwambia, ya kwamba Bwana Mungu wetu anapaswa kutuondokeshea Nabii kama Musa, Naye Ndiye ambaye tulipaswa kumwendea.

⁷⁷ “Basi Simoni, chochote ufanyacho, daima kumbuka, haidhuru kitu chochote kinaonekanaje, kumbuka, Masihi atakuwa ni Nabii, kwa kuwa ni kulingana na Maandiko. Usichukuliwe, Simoni, na mambo ya kipumbavu na mafundisho ya kigeni, bali dumu pamoja na Maandiko, mwanangu. Kwa sababu Musa, kiongozi wetu, ambapo tunajua Mungu alimtura Musa, naye Musa alisema, “Masihi atakuwa ni Nabii.” Na ishara ya Masihi sasa, hatujawa na nabii kwa mamia ya miaka, lakini siku moja kutakuwako na Mmoja atakayejitokeza jukwaani ambaye atakuwa ni Nabii, na Huyo atakuwa ndiye Masihi, maana tunaingojea siku hiyo.”

⁷⁸ Naye huenda alisema, “Basi, ndugu zangu,” akamkumbatia Andrea, na kusema, “Andrea, unakumbuka wakati ulipoenda kumsikiliza Yohana akihubiri, akinena juu ya Masihi? Vema, nilifikiri lilikuwa ni moja ya makosa haya waliyo nayo wote, kuna *hili* na *lile*, wala sikukusikiliza sana, Andrea.

⁷⁹ “Lakini siku moja wakati hatimaye uliponishawishi kwenda kumwona Jamaa huyu ambaye alikuwa, ametambulishwa kama Masihi, basi nilipoenda kumwona, ndugu, nilipoenda mbele ya Mtu huyu, basi Andrea akipanda kilimani alisema, ‘Huyo Ndiye. Mnamwona Yule?’

“Mbona, Yeye haonekani tofauti na mtu mwingine yeyote,’ nilimwambia Andrea.

⁸⁰ “Lakini akasema, ‘Hebu kidogo, hebu tupenye kwenye umati. Anajitayarisha kuzungumza hivi punde tu, na kila mtu atastaajabu sana wakati Yeye akizungumza.’ Basi tukapenya kwenye umati. Naye Andrea alikuwa...alimwona Yohana akimtambulisha. Na kwa hiyo basi nikasogea karibu, nami nikawazia, ‘Ni—nitamwona, nimtazame vizuri, nami nitasikia Yale Yeye asemayo, nione kama anaambatana na Maandiko.’

⁸¹ “Kwa hiyo nikasogea karibu siku hiyo. Wakati alipokuwa tayari kuzungumza, ndipo nikawazia, ‘Sasa, nitaona tu kile Andrea amekuwa akizungumzia,’ na wakati Yeye, kabla hajafungua kinywa Chake kusema lolote, amenikazia macho Yake, Naye akaniangalia na kusema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’ Loo, ndugu, hi—hilo lilinitosha.

⁸² Sio tu kwamba Yeye alijua mimi nilikuwa ni nani, alimjua maskini yule baba yangu mtauwa ambaye alikuwa amenionya na kuniambia kile Masihi angekuwa. Kwa hiyo, nilijua ya kwamba Huyo alikuwa ni Nabii wa Mungu, Masihi aliyeinuliwa. Hilo liliukamilisha huo ushuhuda kwangu.”

⁸³ Hapana shaka ilikuwa ni Filipino yapata wakati huo, aliyesimama na kusema, “Sasa, Ndugu Nathanaeli, nitasimulia hili juu yetu sasa, katika mkutano wa ushuhuda, huku nje baharini.” Hivi si ungalipenda kuwa umesimama, ukiusikiliza huo, umeketi kwenye demani ya mashua, ukiwasikiliza?

⁸⁴ Naye Filipino huenda alisema, “Vema, nilikuwa nimesimama pale, Simoni, nilipomwona akifanya hivyo, ama, kumsikia. Nami nikaona sura ya uso wako, ulianguka tu moja kwa moja miguuni Pake. Ndipo nikawazia, ‘Hakika kwamba huyo mtu mkubwa, mnene, Simoni, angeinamisha tu mabega yake chini.’ Naye akakwambia jina lako litakuwa ‘Jiwe Dogo’ baada ya haya.

⁸⁵ “Nami nilijua hilo lingekuwa ni jina zuri linalofaa kwako, kwa sababu ulikuwa imara. Wakati ulipoamini chochote, ulikiamini. Ndipo nikawazia, ‘Angepataje kujua hilo?’ Kwa hiyo, nilikuwa nimeyasoma Maandiko, pia. Kwa hiyo, nilimjua rafiki yangu mwema aliyeketi hapa mwishoni mwa mtumbwi, ambaye ni Nathanaeli, kwa hiyo nikauzunguka ule mlima mbio kumtafuta.

⁸⁶ “Nami nikamkuta chini ya mti akiomba. Basi alipomaliza maombi yake na alikuwa amesimama, nilisema, ‘Njoo, umwone Mtu tuliyemwona, Yesu, Mwana wa Yusufu, Huyo ndiye Masihi.’

“‘Loo sasa,’ akasema, ‘laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?’

“Nami nikamwambia, ‘Njoo, uone.’

⁸⁷ “Nanyi mnakumbuka mazungumzo yetu barabarani. Na mara nilipomleta Nathanaeli Uweponi mwa Bwana wetu, Yeye alisema, ‘Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!’ Hebu niwaambie, nitakomesha ushuhuda wangu sasa. Sasa, Nathanaeli, malizia.”

⁸⁸ “Vema,” akasema Nathanaeli, “Mimi... Shaka yote iliondolewa kwangu. Lakini nilishangaa mara nilipomwona huyo Mtu, mara ya kwanza niliyopata kumwona, ambapo aliniambia ya kwamba nilikuwa Mwisraeli, wala sina hila. Huyo Mtu angewezaje kunijua, wakati sikuwahi kumwona maishani mwangu, mpaka nilipokuja kwenye mkutano Wake? Nami nilifikiri ningehoji, nami nilikuwa na shauku kubwa kuwazia, ‘Hivi hizi habari zinaweza kuwa ni za kweli, ama—ama nilikuwa tu ninaota ndoto?’

⁸⁹ “Kwa hiyo nikasema, ‘Rabi,’” ama Kasisi, Mwalimu, chochote mnachotaka kuliita, “‘ulipata kunijua lini Wewe? Mbona, hujawahi kuniona maishani Mwako. Basi ungejua ya kwamba nilikuwa mtu mwaminifu, mwenye haki, asiye na hila?’

“Akasema, ‘Mbona kabla Filipino hajakuita, nilikuona, ulipokuwa chini ya mti.’

⁹⁰ “Ndugu, nilijua wakati huo *Huyo* alikuwa ndiye Nabii ambaye tumekuwa tukimtazamia miaka hii yote. Nami

nikamkiri hadharani mbele ya kuhani wangu na wengine wote, nikijua ya kwamba ningetengwa na kanisa kwa kusema jambo kama hilo, ama kuchukua msimamo. Lakini haikuleta tofauti yoyote kwangu, nilijua Maandiko yalisema angekuwa ni Mtu wa aina hiyo.

⁹¹ “Kwa hiyo nikadumu na yale Maandiko yaliyosema, maana Musa, tulifundishwa kumwamini Musa na manabii, nao walisema ya kwamba Masihi huyu angekuwa ni Nabii, wala hatujaona chochote Chake kwa mamia ya miaka, naye Huyu papa hapa pamoja nasi, na mimi—mimi najua huyo Mtu hakunijua, kwa hiyo ilitosha kwangu.”

⁹² Na yapata wakati huo hapana shaka Andrea alisimama na kusema, “Ndugu, ningetaka kusema jambo lingine. Mnakumbuka ile siku aliyosema atashuka kwenda Yeriko?”

“Naam.”

⁹³ “Naye alikuwa na haja, kupitia Samaria. Nasi sote tukashangaa, ‘Kwa nini anapanda kuzunguka huko Samaria, badala ya kushuka kwenda Yeriko?’ Lakini alikuwa na haja ya kupitia kwa Wasamaria. Nanyi mnajua hatukuwa na uhusiano wowote nao hata kidogo.

⁹⁴ “Lakini alisimama, nasi tulifikiri labda hakutaka kuonyesha uso Wake huko Samaria, kwa hiyo akaketi kisimani, kisha akatutuma huko ndani kununua chakula. Ndipo tuliporudi, mnakumbuka tuliyoona? Tulitahayarika, Bwana wetu alikuwa akizungumza na mwanamke mwenye sifa mbaya, msichana mrembo, lakini alikuwa mwanamke mbaya. Alikuwa amesimama huko nje akiwa na alama ya mwanamke mbaya, akija kisimani wakati huo wa mchana, Naye alikuwa akizungumza naye. Mnakumbuka yale aliyosema?”

⁹⁵ “Akasema, tulijificha nyuma ya kichaka kusikiliza na kuona kile alichokuwa akisema, tuone kile Bwana wetu angemwambia mwanamke huyu mwenye sifa mbaya,” kisha kasema, “Alisema, ‘Mwanamke, nipe maji ninywe.’

“Akasema, ‘Si kawaida kwenu Wayahudi kutuomba sisi Wasamaria vitu kama hivyo, hatuna uhusiano sisi kwa sisi.’

“Akasema, ‘Lakini kama ungalijua ni Nani uliyekuwa unazungumza naye, ungeniomba Mimi maji unywe.’

“Naye akasema, ‘Huna kitu cha kuchotea.’

“Ndipo Bwana wetu akasema, ‘Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.’

“Akasema, ‘Sina mume.’

⁹⁶ “Je, mnakumbuka, ndugu, jinsi tulivyojisikia? ‘Uh-loo. Sasa Yeye ameteleza, amefanya kosa. “Sina mume.”’ Ndipo tukayasikia Maneno Yake, ‘Umesema vema, kwa kuwa umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.’

Na halafu mnamkumbuka mwanamke yule Msamaria, wa mji wa Sikari kule, yale aliyosema?

⁹⁷ “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Sasa, sisi Wasamaria tunajua ya kwamba yuaja Mtiwa Mafuta, anayelitwa Kristo, Masihi. Na wakati . . . Tunajua ishara Yake itakuwa nini, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake, Yeye atakuwa ni Nabii. Atakapokuja, atatuonyesha mambo haya. Lakini u Nani Wewe? Wewe hapana saka ni mmoja wa watumishi Wake.’

“Akasema, ‘Mimi Ndiye.’

⁹⁸ “Loo, jinsi tulivyoona sura kwenye uso wa mwanamke huyo, wakati alipoweka chini ndoo yake ya maji na kukimbia mjini na kuanza kupiga mayowe, ‘Njoni mwone Mtu ambaye ameniambia mambo yote ya maisha yangu.’”

⁹⁹ Sasa, kamwe hakumwambia mambo yote, Yeye alininii tu, mwanamke alifurahi *sana*, Yeye alimwambia tu jambo moja, lakini kama alijua jambo hilo moja, Yeye alijua mambo yote. Mnaona? “Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo yaliyo maishani mwangu. Haimkini hii ndiyo ishara halisi ya Masihi? Naye ameketi pale *pale* kisimani.”

Na wakawaleta hao watu huko nje. Nayo Biblia inasema ya kwamba mji mzima ulimwamini Yesu kwa sababu alimwambia huyo mwanamke kitu hicho.

¹⁰⁰ Hapana shaka ilikuwa ni mwandishi Mathayo, akiandika ushuhuda huu, ili nipate kuwasomea usiku wa leo, mnaona, akasema, “Naweza kuzungumza sasa ndugumu?”

“Loo, naam, Mathayo, endelea, zungumza.”

¹⁰¹ “Mnakumbuka ile asubuhi tulipokuwa tukienda Yeriko? Naye Rebekah, dada yetu huko chini Yeriko, alikuwa mke wa Zakayo. Naye alikuwa ni mfanyabiashara, mtoza ushuru mjini, naye alikuwa ni tajiri. Nanyi mnajua Rebekah alimwamini Bwana wetu.

¹⁰² “Naye alikuwa ameomba, naye alikuwa amemwombea mumewe awe Mkristo. Lakini bila shaka, alikuwa mmoja wa watoaji wakubwa kanisani, na—naye alicheza gofu pamoja na makuhani,” mwajua, mnaelewa ninalomaanisha, “a—alikuwa na shughuli zake za kijamii, wote wakatoka pamoja na—na walikuwa na wakati wao mzuri sana pamoja. Kwa hiyo ilikuwa ni vigumu kwake kujiondoa kwenye uanachama wake. Na kwa hiyo, mnajua wao . . . mtu yeyote anayemfuata Bwana wetu ametengwa na makanisa sasa hivi, mnaona. Hawana uhusiano wowote nao.

“Na kwa hiyo, na sisi—sisi tuliombwa na dada yetu, Rebekah, kumwombea Zakayo, mumewe, kwamba angempokea Bwana wetu.

¹⁰³ “Nanyi mnakumbuka tuliposimama pembeni na kumwambia Zakayo, ‘Zakayo, wewe ni msomaji wa Biblia,

unatafuta nini? Wasemaje juu ya Masihi? Ushuhuda wa Rebekah ni wa kweli, Yeye ndiye Nabii ambaye Bwana Mungu wetu alikuwa anaenda kumwinua katika siku hizi.’

¹⁰⁴ “‘Loo, lakini Rabi Lavinski anianiambia ya kwamba Yeye ni nabii wa uongo, Yeye ni—Yeye ni Beelzebuli, Yeye—Yeye amepagawa roho ya kupiga ramli. Sitaamini hilo,’ anaondoka.

¹⁰⁵ “Nanyi mnakumbuka ushuhuda wa Rebekah siku ile? Jinsi yeye—yeye alivyosema wakati Zakayo alipoamka mapema asubuhi hiyo, naye alikuwa ameomba usiku kucha kwamba Zakayo angeweza kumwona Yesu alipokuja mjini.”

¹⁰⁶ Sasa, enyi wanawake, hiyo ndiyo njia ya kumfanya mumeo avutiwe kwa Mungu, inahitaji kuomba kidogo, kushikilia. Usiku kucha aliomba. Ndipo kesho yake asubuhi, alijua ya kwamba Yesu alikuwa anaenda kuutembelea huo mji siku hiyo. Kwa hiyo yeye—yeye, usiku kucha alikuwa ameomba ya kwamba Zakayo angeona namna fulani ya mwujiza ambao Yesu angefanya, ambao ungeubadilisha moyo wa mumewe. Nanyi mwajua, tunafundishwa hivi, enyi marafiki: Kuomba kwa imani kutafanya mambo makuu. Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.

¹⁰⁷ Ndipo basi huenda Mathayo alisema, “Nanyi ndugu, mnakumbuka asubuhi ile tulipokutana na Rebekah? Alisema, ‘Niliomba usiku kucha. Na asubuhi ya leo yapata mapambazuko, vema, Zakayo aliamka mapema, akavaa vazi lake lililo bora zaidi na kuchanua ndevu zake, mwajua,’ maana alikuwa mtu mashuhuri, ‘kwa hiyo akavaa nguo zake zilizo bora zaidi, mwajua. Ndipo nikasema, “Unaenda wapi, Mpenzi?””

““Loo, kwa matembezi tu ya asubuhi.” Hilo halikuwa la kawaida mwajua, kwa sababu hakuamka mapema hivyo.’

¹⁰⁸ “Kwa hiyo Rebeka akashuka sakafuni na kusema, ‘Asante, Bwana, najua Wewe unamshughulikia,’” mnaona, “kwa sababu amekuwa akilalamika sana siku chache zilizopita.” Mnaona? Kwa kawaida hiyo ni wakati Yeye akiwa njiani, mnaona. “Loo, amenikatilia mbali na kila kitu, bali ninajua ya kwamba Wewe utamwongoza kwa namna fulani moja kwa moja hadi mahali Yesu alipo.’

¹⁰⁹ “Vema, sasa mnakumbuka tulichukua...Naye alikaa nyumbani kuomba. Kwa hiyo mnakumbuka yale Zakayo aliyotwambia baada ya hadithi hiyo? Alisema kote moyoni mwake, usiku kucha alikuwa ameota ndoto ya kumwona Mungu akimshughulikia.

¹¹⁰ “Basi kesho yake asubuhi alipoamka, alitoka akashuka pembeni mwa lango la upande wa kusini wa mji, ambako alikuwa atokee, ndipo alipofika kule, kufikia mapambazuko Wagalilaya walikuwa wamesongamana kila mahali malangoni kumngojea.

111 “Vema, alikuwa ni mtu mdogo, kwa hiyo, a—alikuwa ni mdogo wa kimo, naye akasema, ‘Mimi ni mfupi sana kamwe siwezi kuingia katika kundi kama hilo, kamwe nisingemwona. Lakini nitamwambia ukweli wa mambo nitakapomwona. Nitamwambia Yeye ni nabii wa uongo, Yeye si mwonaji.’

112 “Kwa hiyo ilitokea aliwazia, ‘Unajua, mimi, kama akija humu ndani, sitamwona. Lakini ninajua Yeye anaenda kwa Lavinski, kule, kwa chakula cha kutwa, mshindani wangu. Kwa hiyo ni—niwaambie nini, nitapanda hapa juu, nami najua Yeye atapitia kwenye Barabara Kuu ya Haleluya, ambapo inashuka kwenye Barabara ya Utukufu, na,’” kwa kawaida Yeye hupitia njia hiyo, mwajua, “‘kwa hiyo nitapanda kwenda kule na kusimama kule juu. Basi atakapopita, nitamwona.’

113 “Vema, akasimama pale naye alikuwa amejinadhifisha vizuri sana, kasema, ‘Nitasimama papa *hapa*, ndipo atakapokuja, nitasema, “‘Rabi, nimempiga mke wangu kofi kutoka kitandani siku nyingi usiku, kwa sababu Yako. Nataka uachane naye! Ninamtaka arudi kanisani pamoja na makundi ya kina mama ya kushona na yote hayo.’” Mnaona? “‘“Mbona, mimi ni mfanyabiashara aliyetahayarishwa katika jiji hili, kwa sababu amekuwa akifuatana na kundi la walokole, kundi la watakatifu wanaojifingi- . . . , ama, wajua, watu kama Wewe.’” Mnaona? “‘“Kwa hiyo mimi ni . . . na—na—nataka uondoke humu nchini.” Nitamwambia, jamani, na kila mtu atajua mimi ni—mimi ni . . . Mimi ni jamaa *fulani*, nina akili kweli,’” mnaona.

114 “Naye alikuwa amesimama pale pembeni, ikatokea tu aliwazia, ‘Vema, unajua nini? Umati huo utamfuata.’” Hiyo ni kweli, wataamfuata. “‘Popote aendapo, wataenda pia. Mnajua nini? Mimi ni mdogo sana, watakapofika hapa juu, huenda wakanikanyagia chini. Kwa hiyo kuna ninii tu. . . Sijui jinsi ya kulifanya.’

115 “Kwa hiyo akaangalia na kulikuwa na mti wa mkuyu umesimama pale, akawaza, ‘Vema, unajua nini? Ninaamini nitaupanda *huo*. Ndipo nitakapofika huko juu, sasa, ninafanya haya yote kwa sababu gani? Kwa hiyo mimi, lakini kama nikifika kule juu, nitamwona atakapopitia hapa, nami nitamtolea hotuba kutoka juu ya mti huu.’

116 “Kwa hiyo akaangalia kote, naye alikuwa mfupi sana asingeweza kulifikia hilo tawi, mwajua. Lakini alikuwa amekusudia kumwona.” Kama umekusudia, Mungu atakuandalia njia ya kumwona Yeye vizuri, unaona. Wewe kusudia tu, unaona.

117 “Na kwa hiyo akaangalia kila mahali, ikatokea aliwazia, ‘Vema, ni nini . . . ? Vema, mwokota takataka hakuwa amekuja bado asubuhi ya leo.’ Nayu ndoo ya takataka ilikuwa imewekwa pale. Kwa hiyo anaenda kule kuichukua hiyo ndoo ya takataka, nayo ilikuwa nzito mno. ‘Vema, hakuna kitu kingine hapa,

ila ninataka kumwona Yeye.” Loo, utafanya mambo ya kigeni wakati unapotaka kumwona. Unafanya mambo usiyofikiria ungefanya, mambo ya aibu.

118 “Kwa hiyo anaikumbatia hiyo ndoo ya takataka, huyu hapa anakuja sasa, na yapata wakati huo, hawa hapa wafanyabiashara wawili au watatu wanakata kona, washindani wake, basi amenaswa katika mtego.” Labda baadhi yenu mko katika hali iyo hiyo usiku wa leo, mmenaswa miongoni mwetu sisi watakatifu wanaojifingirisha, kwa hiyo haya basi, afadhali uichukue tu, unaona.

119 “Kwa hiyo hao hapo, alikuwa ameshika ndoo, maskini uso wake ukawa mwekundu, bali hakujali, anaenda kumwona kwa vyovyote vile.” Hiyo ndiyo njia. Sasa, Zakayo, sasa unakuwa sawa. “Anaibeba na kuiweka chini karibu na ule mti. Na kuparamia juu ya . . .” Simaanishi kusema hivyo. Tunakuita huko Marekani *kuparamia mti*, mwajua, ni “kurukia mti, na kuupanda.”

120 “Akapanda huko juu. Akafika . . . Akaketi ambapo matawi mawili yanakutana, namna *hii*, akaketi chini kwenye matawi hayo.” Hapo ni mahali pazuri pa kuketi kidogo, ambapo njia mbili zinakutana, yako na ya Mungu. Liwaziendi kidogo. Utakufa moja ya siku hizi. Huna budi kukutana na Mungu aliyeliandika Neno hili, huna budi kuliwajibikia moja ya siku hizi. Kwa hiyo natumaini ya kwamba kuna Zakayo wengi waliopo hapa usiku wa leo, watakaoketi kwenye makutano hayo usiku wa leo, kata kauli.

121 Jinsi alivyokuwa na sura ya kusikitisha, ameketi pale akichokoa vibanzi kutoka kwake, suti yake mpya imejaa takataka, na, bali alikuwa amekusudia kumwona Yesu, mnaona. Alitaka kumwona.

122 “Kwa hiyo akaanza kuwazia, ‘Mwajua, ni kitu gani kinachonifanya nifanye hivi? Mwajua, Rebekah aliniambia ya kwamba Jamaa huyo alikuwa ni nabii, kwamba angeweza *kuona*. Sasa, siamini hilo, hakuna kitu kama hicho katika siku hii, kuhani wangu aliniambia hakuna manabii wa siku hizi. Manabii walikuwako mamia ya miaka iliyopita, huko nyuma kabisa, wakati wa Musa, bali hakuna manabii siku hizi. Kwa hiyo, mnajua ninachoamini? Hapo awali, kabla sijamwambia mawazo yangu, ninaamini nitajifunika tu, kusudi asiweze kuniona.’ Kwa hiyo akashika matawi yote, na kujifunika, akajificha kusudi asionekane na mtu yeyote.

123 “Kwa hiyo akajiachia jani moja kubwa namna *hii*, kama mlango, angeweza kuliinua chini na kuangalia nje. Ndipo akaketi pale akishangaa, ‘Sasa, Yeye kamwe hatajua niko huku juu, maana hawezi kuniona juu ya mti huu, nami nitaona tu kwamba Yeye ni *nabii* kiasi gani.’ Na mara kwa mara, angeweza kusikia makelele.” Mwajua, kwa kawaida mahali Yesu alipo,

kuna kelele nyingi sana, sijui ni kwa nini, lakini kwa kawaida ndivyo ilivyo, mnaona.

¹²⁴ “Na kwa hiyo akalishusha hilo jani, akaangalia juu ya hilo jani, hakuna mtu anayekuja. Baada ya kitambo kidogo, akasikia makelele, akaangalia chini na barabara zilikuwa zikianza kuwa na msongamano wa watu. Akachungulia chini ya jani, mwajua, akiangalia, akiangalia huku na huku apate kuona, baada ya kitambo kidogo, mtu mkubwa mno mwenye nguvu akapiga kona, barabara imejaa watu, ‘Samahani sana asubuhi ya leo, marafiki, hivi mnaweza kurudi nyuma na kumpa Bwana wetu nafasi? Yeye ni—Yeye ni mchovu sana na amedhoofika. Amekuwa macho usiku kucha, amekuwa akiwaponya wagonjwa jana, na mambo yamefanywa. Mwaweza kurudi nyuma tafadhali?’

“Huyo hapana shaka ndiye Rebeka alisema alikuwa ni Simoni Petro. Anaonekana kama jamaa mkubwa, mwenye misuli mikubwa.’

“Mwaweza kusimama . . . ?”

“Hawa hapa watu wengine wanakuja nyuma, “Tunasikitika sana, lakini mpeni Bwana wetu nafasi, sivyo? Kwa sababu amechoka sana asubuhi ya leo.”

¹²⁵ “Vema, nikawazia, “Sasa, Yeye kamwe hataniona nimeketi hapa.” Na kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, nikaangalia pembeni, na hapo alisimama ra—rafiki yangu akiwa na mtoto mchanga mgonjwa, ambaye hivi punde tu nimekuwa kule chini na kuzungumza naye, naye daktari anayekula kwenye mkahawa ule ule wangu, ambamo mimi na kasisi tunakula, alimwambia mwanamume huyo kwamba mtoto huyo mchanga angekufa wakati wowote, na homa yake ilikuwa kali sana, nao hawa hapa wamejifunika blanketi, wamesimama huko nje kumwona huyu Mlokole akija huku.’

¹²⁶ “Baada ya kitambo kidogo, maskini huyo baba akakimbia mbele Zake, akaanguka chini, na kusema, “Waweza kumrehemu mtoto wangu mchanga?” Naye akagusa tu ile blanketi, msichana huyo mdogo akaanza kuruka na kukimbia, akiondoka.’

¹²⁷ “Ndipo alipoangalia chini, kulikuwa na kitu fulani kuhusu Mtu huyu, Yesu, hata wakati alipomwona, alibadilisha nia yake, hakujisikia kumkemea.” Kama ukipata kuangalia moja kwa moja katika Maandiko na kumwona Yesu, kile alichu, hutamkosoa tena.

¹²⁸ “Hakutaka kumpigia makelele, bali aliliinamisha hilo jani dogo chini na kuanza kumwangukia akija, alikuwa ameinamisha kichwa Chake, akitembea imara.” Biblia ilisema hana uzuri hata tumtamani, kwa hiyo labda alikuwa ni Jamaa mdogo, mwenye mabega yaliyoinama, akitembea mitaani.

¹²⁹ “Basi alipofika moja kwa moja chini ya mahali alipokuwa, alisimama, naye huyu hapa alikuwa akichungulia juu ya jani

hili, akaangalia juu, kasema, ‘Zakayo, shuka chini; ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa chakula cha kutwa leo.’ Si kwamba tu alijua alikuwa kwenye mti, bali alijua alikuwa ni nani. ‘Zakayo, shuka, harakisha, shuka uje mara moja, Rebekah anatungojea.’

“Mnakumbuka jinsi Yeye . . . ?”

¹³⁰ “Loo, naam,” wote wakasema, “Ninakumbuka hilo, naam, bwana. Tunakumbuka ushuhuda huo, yale Zakayo aliyosema kule juu siku ile kwenye chakula cha kutwa, jinsi alivyoona aibu na kusema, ‘Bwana, kama nimefanya kosa lolote, nitalirekebisha. Ninajua ya kwamba Wewe ndiwe Masihi, hakika, nimeridhika, ulipoliita jina langu, mimi nikiketi pale juu kwenye mti ule.’”

“Loo, naam.”

¹³¹ “Na kusema, tulipotoka malangoni, mnamkumbuka maskini yule Bartimayo Kipofu, alikuwa huko nje upande wa pili kule? Mnakumbuka ushuhuda wake, ndugu?”

“Naam, ninakumbuka.”

¹³² “Alikuwa ameketi pale akiota juu ya siku ambazo angeweza kuona, wakati alipokuwa na uwezo wa kukimbia huku na huku, na kuchuma maua madogo kwenye kilima cha Uyahudi.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹³³ Lakini Yeye hamfanyii ibilisi vitimbi. Akasema, “Sifanyi lolote mpaka Baba . . .” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “. . . ? . . . lile nimwonalo Baba akilitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.” Ni wangapi wanaojua Maandiko hayo? Yohana Mtakatifu mlango wa 5.

¹³⁴ Wakati Yesu alipopitia kwenye birika la Bethesda na kumponya mtu mmoja, akaacha umati wa watu, maelfu wamelala pale, vilema, vipofu, waliopindika, waliopooza, Yeye alimwendea mtu ambaye labda alikuwa na ugonjwa wa tezi kibofu, labda alikuwa na TB, ilikuwa imedumaa, alikuwa nayo kwa muda wa miaka thelathini na minane, kwa nini Yeye hakuwaponya wale waliokuwa viwete na vipofu? Alipitia moja kwa moja miongoni mwa kila mmoja wao akamwendea jamaa huyu.

Sasa, kumbukeni Biblia ilisema Yesu alijua ya kwamba alikuwa katika hali hii, mnaona. Naye akasema, “Wataka kuwa mzima?”

Kasema, “Sina mtu wa kunitia majini.”

Kasema, “Jitwike godoro lako.”

Kasema, “Mtu mwingine anaweza kushuka mbele yangu.” Angeweza kutembea, kasema mtu mwingine anamshinda mbio, anashuka kule kwanza, anaingia majini wakati malaika alipoyatibua hayo maji.

Kasema, “Jitwike godoro lako uende nyumbani kwako.”

¹³⁵ Naye akaulizwa. Kama angefanya hivyo katika mji huu, usiku wa leo, angeulizwa. Mwangalie ibilisi akisema, “Tuna mtu anayeuzua penseli hapa chini mitaani, kipofu. Hebu hawa waponyaaji wa Kiungu wamponye.” Mnaona? Mnaona, huyo ibilisi? Yule yule aliyesema, “Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, fanya mwujiza mbele zangu, geuza mkate huu katika . . . mawe haya yawe mkate. Nitakuamini.”

¹³⁶ Ibilisi yule yule, walipokuwa wamempeleka mahakamani, walimfunga kitambaa kichwani Mwake, na kundi la askari walevi likampiga kichwani kwa fimbo, kasema, “Kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga. Tutakuamini.” Mnaona? Mungu hafanyi vitimbi.

¹³⁷ Yesu alisema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile *amwonaldo* Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.” Haya basi, huyo hapo mtumishi halisi wa Mungu. “Siwezi kufanya neno Mwenyewe ila lile nionalo,” si *nisikialo*, *nionalo*. Basi Yesu hakutenda jambo moja mpaka Mungu alipomwonyesha kwa ono jambo la kutenda, la sivyo Yeye alisema jambo baya katika Yohana Mtakatifu 5:19.

¹³⁸ “Amin, amin,” hiyo ni *kabisa*, *kabisa*, “nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe,” huyo alikuwa ni Mwana, u—ule mwili ambao Mungu aliishi ndani yake, “Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile nimwonaldo,” *kuona* “Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile. Baba anatenda kazi nami ninatenda kazi hata sasa.” Kwa maneno mengine, “Baba hunionyesha la kufanya, nami ninaliigiza tu kama mchezo wa kuigiza.”

Sasa, Bartimayo Kipofu alisema pale, kasema, “Ni nani anayepita?”

¹³⁹ “Loo,” wakasema, “nyamaza,” wakamsukumia mbali. Na hapo, hatimaye maskini mwanamke mwema, mtumishi wa Kristo . . . Watumishi wote wa Kristo ni wema. Mnaamini hilo? Wanapenda kuwaonyesha heshima wale walio wahitaji, kuwasaidia vipofu kuvuka barabara, kuwaleta mkutanoni, kufanya mambo mema. Wakati jirani ni mgonjwa, wanaenda kuwasaidia, kamwe hawatarajii pesa, kuwafadhili wengine. Watumishi wote wa Kristo wako hivyo, wanapenda kuwasaidia wale waliopungukiwa na kukanyagiwa chini.

¹⁴⁰ Maskini huyu kipofu, aliyesukumia wale, huku wote wakipiga makelele, mmoja akisema, “Salamu, Salamu, *hapo*, Mfalme, Nabii, Nabii wa Galilaya, salamu Kwake!”

Mwingine akisema, “Mwondoeni huyo mwigaji!”

¹⁴¹ Wengine wanasema, “Njoo ukawafufue wafu, ewe mnafikiki. Wengi sana wamelala hapa juu kilimani, njoo huku ukamfufue mmoja wa watu wetu. Tulikuwa na kuhani mtauwa aliyekufa

juma lililopita, njoo, ukamfufue kama wewe ni Mwana wa Mungu.”

¹⁴² Yesu kamwe hakufungua kinywa Chake, aliendelea tu kutembea. Ninii yote. . . Alikuwa akienda Kalvari, papo hapo, akipanda kwenda Yerusalemu, mzigo wa ulimwengu ulikuwa juu Yake, kila mtu aliyewahi kufa, kila dhambi iliyowahi kutendwa iliwekwa juu Yake, Naye alijua alikuwa anaelekea mautini.

¹⁴³ Ninaweza kumsikia Bartimayo akisema, “Ni nani anayepita hapa?” Hakuna mtu angemwambia.

Mara, maskini mwanamke huyu mwema akasema, “Bwana, hebu nikusaidie kusimama, bwana mwenye fadhili.”

“Loo, wewe ni mama mzuri. Wewe ni nani?” Akamwambia. . .

Akasema, “Mimi ni mtumishi wa Kristo.”

“Ati wa *Nani*?”

“Kristo. Je, wewe ni. . . ? Wewe ni Myahudi?”

“Naam.”

“Kwani hujasoma katika Maandiko ambapo Masihi alikuwa anakuja?”

“Loo, yule Mwana wa Daudi?”

“Naam. Yeye atakuwa ni mtu wa aina gani?”

“Loo, Yeye atakuwa ni Nabii,” kasema Bartimayo Kipofu. “Yeye atakuwa ni Nabii.”

“Huyo Ndiye ambaye amepita sasa hivi.”

“Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!”

Baadhi yao wakasema, “Nyamaza.” Angeweza je kusikia hilo?

¹⁴⁴ Nenda Yeriko wakati mmoja uone mahali alipokuwa ameketi na mahali Yesu alipokuwa, yapata yadi mia tatu. Maelfu ya watu wakisema, “Salamu Nabii!”

Mwingine akisema, “Mwondoeni huyo mnafiiki!” Akatupiwa vyakula vilivyooza, na kila kitu namna hiyo, “Ondoka mjini mwetu!” Mnaona?

Na wengine wakimbariki, na wengine wakimlaani, jambo lile lile leo hii, jambo lile lile.

Wengine wanasema, “Ni kweli, ni ya Mungu.”

Huyo mwingine akasema, “Ni ibilisi.”

¹⁴⁵ Haya basi. Mnaona? Mungu humchukua mtu Wake bali kamwe si Roho Wake; ibilisi humchukua mtu wake bali kamwe si roho, kwa namna fulani tu anaendelea kuishi ndani ya mtu mwingine, anaendelea tu kurudi, kama Roho Mtakatifu. Mnaona? Sasa, wote wawili wanaishi leo, wote wawili wanaishi

katika Grande Prairie, mnajua hilo. Hakika, wanaishi, roho zote mbili. Wao . . . Popote wanadamu wanapokusanyika pamoja, unakuta roho zote mbili.

¹⁴⁶ Hawa hapa, na sasa, pale . . . Yesu asingeweza kumsikia kihalisi, ni kelele nyingi mno. Lakini hapana shaka Bartimayo Kipofu alisema hivi: “Basi najua ya kwamba Huyu ndiye yule Masihi niliyejua atakuja, nami ninajua ya kwamba Yeye ni Nabii.” Kwa hiyo hapana shaka alipiga magoti na kusema, “Yehova, Yehova!” Mnaona, inalingana na Maandiko mengine, yule mwanamke aliyegusa vazi Lake. Yeye ni Kuhani Mkuu usiku wa leo, ambaye unaweza kugusa vazi Lake.

¹⁴⁷ “Yehova, mimi ni kipofu, sina pesa kwa ajili ya upasuaji, wala hawangenifaa kitu kwa vyovyote vile. Yehova, Huyu ni Mwana wa Daudi Naye anapita, unirehemu!” Imani Yake ikamsimamisha, imani ya ombaomba kipofu, mtu asiye na maana.

¹⁴⁸ Si kilio chake, Yeye asingeweza kukisikia, zilizidi sana, mmoja akisema *hivi*, na huyo mwigine jambo lingine, bali imani yake ilimsimamisha, maana Yesu alisema hivyo. Pia kumbukeni, huku dhambi za ulimwengu zikiwa juu Yake, akienda zake Yerusalemu, imani ya ombaomba mmoja ilimsimamisha njiani Mwake.

¹⁴⁹ Laiti ningalikuwa na siku chache, ningependa kuwahubiria usiku mmoja, juu ya kuhubiri tu. “Naye Yesu Akasimama Kimya.” “Jua Likasimama Kimya.” Moja ya siku hizi, wakati utasimama kimya! Lakini Yesu alisimama kimya, akasema, “Imani yako imekuokoa.”

¹⁵⁰ “Basi mnakumbuka yale Bartimayo Kipofu aliyosema? Alisema ya kwamba Huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu, ‘Mtu huyo alikuwa ni Nabii, imani yangu ilikuwa na nguvu vya kutosha kumsimamisha. Nami nikamwomba ayafumbue macho yangu Naye akasema, “Imani yako imekuokoa.” Nikasimama nikiangalia, umati ukashuka barabarani, nikasema, “Haina budi kuwa hivyo, haina budi kuwa hivyo, ninajua ndivyo ilivyo.” Ndipo baada ya kitambo kidogo nikaanza kuona kivuli, nikaanza kuona, na hiyo hapo mikono yangu, mimi, nikikimbia barabarani nikifurahi.”

“Loo, hakika.”

¹⁵¹ Loo, ni mkutano wa ushuhuda wa jinsi gani waliokuwa nao! Hapana shaka walikuwa wakilia na kupaza sauti na kurukaruka ndani ya chombo, wakipiga makelele, “Utukufu kwa Mungu! Mungu asifiwe, Ndugu! Tunajua tuko sahihi, tunajua ya kwamba Yeye ndiye Masihi.”

¹⁵² Ndivyo ilivyo siku hizi, unaweza kuchukua theolojia yako yote iliyokufa unayotaka, nitamchukua Kristo aliye hai. Uhuh. Kwangu mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Mungu.

Loo, napenda tukio, Urimu na Thumimu, Neno la Mungu lililofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, huyo ni mimi.

¹⁵³ Mkutano huo wa ushuhuda, yapata wakati huo, tukaanza kuona, hapana shaka ibilisi aliangalia juu ya kilima cha Galilaya, na kusema, “Loo, hao *hapo*, huko nje wakiwa na mkutano wa ushuhuda, bali wameondoka bila yeye, yeye hayuko pamoja nao sasa. Kwa hiyo ikiwa hayuko pamoja nao sasa, huu ndio wakati wangu wa kuwakamata.”

¹⁵⁴ Ndugu zangu wa thamani, hivyo ndivyo angeweza kusema tena. Makanisa yanaondoka bila Yeye. Wanaenda kwa shamrashamra kubwa za kimadhehebu, ndugu zetu wa Kipentekoste wanaenda, wakijaribu kupata washiriki wengi kuliko *hili*, ama washiriki wengi kuliko *lile*, wakiwa na mipango mikubwa inayoendelea, mambo makuu, wakijaribu kujilinganisha na makanisa mengine. Hatupaswi kufanya hivyo. Na tukae pamoja na Yesu.

¹⁵⁵ Ibilisi anasema, “Sasa, nitawazamisha, nimewaona wakienda bila yeye.” Na hilo ndilo tu analojaribu kufanya sasa. Kwa hiyo akaanza kupuliza pumzi yake ya sumu, “*Whiu!*” Maskini hiyo bahari ya kale ikaingiwa na unyong’onyevu wa wasiwasi, hapa mawimbi yakaanza kuruka na kufingirika na kuninii. . . Kasema, “Nitawazamisha sasa,” wamesimama, macho yakimetameta kwenye kila wimbi, na umeme ukimulika, ngurumo zikinguruma. Kasema, “Tutawapata sasa, kwa sababu tumewapata hapa nje bila yeye.”

¹⁵⁶ Hivyo ndivyo ibilisi amelifanyia kanisa siku hizi, limeondoka bila Yesu kwenye shamrashamra kubwa za kimadhehebu. Na muda si muda mwajua, mambo mengine ya ulimwengu na kujaribu kujilinganisha na ulimwengu. Hatuwezi kujilinganisha na ulimwengu. Usiende kwenye eneo la walimwengu ukawaingize watu ndani. Tuna Kitu wasicho nacho. Haleluya! Tunaye Yesu, wana madoido. Tunawezaje kujilinganisha nao kwa madoido? Injili si kumetameta, ni kumeka. Hakika, wala huwezi kuifanya *imeke*, inaingia ndani yako na kumeka yenyewe. Amina. Naam.

¹⁵⁷ Hilo ndilo tunalojaribu kufanya, kuingia katika namna fulani ya hamaki ili kupata wengi kuliko Wabaptisti, ama zaidi ya Wamethodisti, na jinsi ya kuyafanya makanisa yetu yaonekane kama yao, na madhehebu yetu kuwa sawa na yao. Na, loo, upuuzi! Hebu tumrudie Kristo. Hebu turudi kwenye mikutano ya maombi ya mtindo wa kale, turudi kwenye usiku wa kiungu wa machozi na kulia mbele za Mungu, mpaka tutakapomwona Mungu aliye hai akitenda kazi miongoni mwetu, mikutano ya maombi ikiibuka, na watu wakija chini ya sadikisho, kurudi kwenye hilo. Ametushika kwenye hamaki, pia.

¹⁵⁸ Sasa, ni jambo gani lililotukia? Matumaini yote yalikuwa yamekwisha, makasia yakavunjika, tanga likashuka. Lakini

mwajua, sitaki kuwaacha mmekeki huko nje, hatutaki kukaa huko. Lakini mnajua, ni kama tu Yesu, Mfaransa anamwita, “Jésus,” ni kama tu Jésus, Yeye hatakuacha. Mnajua yale aliyofanya? Alijua watapata matatizo, alijua watayapata, jambo fulani lilikuwa linaenda kutukia huko nje. Naye alijua jambo fulani lilikuwa linaenda kutupata, Yeye ni Mungu, Yeye alijua mwisho tangu mwanzo.

¹⁵⁹ Mnajua yale aliyofanya? Alipanda kilima kirefu kuliko vyote vilivyokuwako Palestina. Kadiri unavyozidi kwenda juu, ndivyo unavyoweza kuona mbali zaidi. Kwa hiyo akapanda juu ya kilele cha mlima mrefu zaidi ili aweze kuwaangalia. Walipoingia katika shida na kumhitaji, Yeye angeweza kuwa Msaada unaopatikana tele wakati wa shida.

¹⁶⁰ Na, ndugu, walipomsulubisha pale Kalvari, ulimwengu ulidhani walikuwa wamempata, Mauti ilidhani imempata, Kuzimu ilidhani ilikuwa imempata, ibilisi alidhani alikuwa amempata, lakini alivunja kila muhuri. Yeye hapandi tu kupitia Kalvari, bali kupita kila mwezi na nyota, na ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu, usiku wa leo. Na jicho Lake liko juu ya shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia, sivyo na wewe?

¹⁶¹ Yeye anaona shida yetu, fadhaa zetu, kila kitu kikizunguka *hivi*, na baadhi yao wakijaribu kusema, “Vema, kamwe siamini jambo hilo,” na huyo mwingine akisema *hivi*, maradhi, kansa, magonjwa, mambo ya kila namna, yakiingia miongoni mwa Wakristo, wakienda kombo kwa kutenda mambo ya kilimwengu na kadhalika. Acha tu mjeledi uingie, hivyo tu.

¹⁶² Lakini kumbukeni, Yeye ameketi juu sana, akikuangalia, akiona kile utakachofanya. Moja kwa moja kwenye wakati wa giza sana, wakati matumaini yote ya uamsho yalipokuwa yamekwisha, Huyu hapa akaja akitembea juu ya bahari. Huyu hapa akaja akitembea, juu ya bahari.

¹⁶³ Mnajua nini? Hao wanafunzi ni kama tu watu wengi siku hizi. Huo ulikuwa ndio Msaada pekee ambao wangeweza kupata, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, nao walikiogopa. Wakasema, “Anaonekana kama mzuka. Hapana shaka Yeye ni mpiga ramli. Lazima iwe ni telepathia.” Walimwogopa.

¹⁶⁴ Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, watu hawajui la kufanya kulihusu. Anatembea moja kwa moja miongoni mwetu tena, amina, akitembea miongoni mwetu katika shida, wakati mabomu ya atomiki na kadhalika yakining’inia kila mahali, lakini moja kwa moja katika saa hii yenye giza, wakati makanisa yamechanganyikiwa kabisa na kuvunjika-vunjika katika tofauti za kimadhehebu, Yesu anakuja akitembea moja kwa moja miongoni mwetu, nao watu wanasema, “Sijui, sijui sasa. Halikuja kwenye dhehebu letu, inatubidi kuwa waangalifu,” mnaona.

¹⁶⁵ Lakini hayo Maneno yalikuwa nini? “Ni mimi, msiogope.”

¹⁶⁶ Kwa hiyo usiku wa leo, Grande Prairie, mimi ni ndugu yenu, Yeye ni Bwana wenu, lakini huyo ni Yeye akitenda kazi miongoni mwenu. Ninyi Wapentekoste, hivi Biblia haisemi, hivi Paulo hakusema, “Ninyi nyote mkinena kwa lugha, ndipo akaingia mtu miongoni mwenu asiye na elimu, hakuna tafsiri yake, hivi hatasema mna wazimu? Lakini kama mmoja ni nabii na kufunua siri za moyo, basi wote wataanguka chini, waseme, ‘Hakika, Mungu yuko miongoni mwenu’?”

¹⁶⁷ Mimi si mtu aliyetengwa na jamii, mimi ni ndugu yenu. Kama Yesu angeweza kunena kwa Sauti inayosikika usiku wa leo, mngemsikia akisema jambo lile lile, “Msiogope. Ni mimi, msogope.” Ni Mungu yeye yule, Roho yeye yule. “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona,” mwaminio, “kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Yeye alitabiri katika siku hizi za mwisho, wakati wa jioni, kwamba jambo lilo hilo lingetukia, ambalo tumelipitia juma hili.

¹⁶⁸ “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma . . .” Hiyo ni . . . Ilikuwa nini . . .? Sio katika Nuhu, sasa, kumbukeni Yeye alielezea jambo hilo, bali Sodoma. Na huu ndio wakati wa Sodoma, wakati ulimwengu utateketezwa, sio kuzamishwa, kuteketezwa, utateketezwa. Nayo ishara hii ilikuwa irudi, si safina, bali Mungu akiishi katika miili ya watu Wake, katika Kanisa Lake.

¹⁶⁹ Mnaona, Yesu alisema, “Siku hiyo, mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Ni Mungu ndani yako. Yote aliyokuwa Mungu aliyamimina ndani ya Kristo, na yote aliyokuwa Kristo aliyamimina ndani ya Kanisa. Kwa hiyo ni Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, na Mungu ndani yetu. Si ajabu tumeagizwa kubatiza kwa kutumia Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Si Miungu watatu mbalimbali, ofisi tatu za Mungu mmoja. Mnaona? Mungu juu yetu katika Baba, Mungu ndani, uh, pamoja nasi, katika Mwana, akiisafisha njia Yake, akijidhili, akishuka, akitengeneza njia ambayo angeweza kurudia na kuwarudisha watu Wake wapate kufanywa wana wa Mungu waliodhihirishwa, kama walivyokuwa nao katika bustani ya Edeni. Ulimwengu mzima unaugua na kungojea saa hiyo, kwa ajili ya kudhihirishwa kwa wana wa Mungu.

¹⁷⁰ Hana sauti usiku wa leo ila sauti yetu, hana mikono ila mikono yetu. Yeye ana mikono yako, hiyo ndiyo mikono yake. Alisema, “Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi.” Natumaini ya kwamba mtaisikiliza maskini sauti hii usiku wa leo, na ile Sauti ndogo Tulivu ya Roho inayoweza kunena moyoni mwako, na kumsikia Yeye akisema, “Ni mimi, usiogope.” Mtaamini? Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁷¹ Bwana Yesu, majira yanazidi kuchelewa na kuingia giza. Sijui ni wakati gani Wewe huenda ukaja. Ninaamini ya kwamba umeunyosha mkono Wako mkuu na kuyasimamisha majira, ukayashikilia kwa muda kidogo tu. Sayansi ilisema miaka michache iliyopita, ilikuwa ni usiku wa manane kasoro dakika tatu. Ulisema katika Neno Lako Mwenyewe, “Mtakapoonamambo haya yakianza kutimia: Israeli wakirudishwa, mtini ukichipusha majani yake. . .” Israeli ni taifa sasa. Ile Nyota ya Daudi yenye ncha sita, bendera ya kale kuliko zote ulimwenguni, haijapepea kwa muda wa miaka elfu mbili mia tano, inapepea juu ya Israeli usiku wa leo. Israeli wakirudishwa, lina pesa zake lenyewe, jeshi lake, ni taifa.

¹⁷² Maelfu wakirudi, wakisema, “Yuko wapi huyo Masihi?” Ni fursa ya jinsi gani sasa, tuliyo nayo! Kasema, “Hebu tumwone akifanya ishara ya nabii. Kama tungeweza kumwona akifanya ishara ya nabii, basi tutajua Huyo ni Masihi, kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, aliahidi hilo.” Ee Mungu, wakati Mataifa wanapata wito wao wa mwisho, jalia waisikie Sauti ya Mungu, usiku wa leo, ikisema, “Ni mimi, msiogope.”

¹⁷³ Bwana, nimechoka, nimechoka sana ni vigumu kwangu kusimama hapa. Ninaomba ya kwamba utatufanyia jambo fulani maalum usiku wa leo. Tujalie, Bwana, fanya jambo fulani jinsi tu ulivyolifanya. Chukua ushuhuda hapa baada ya miaka elfu moja mia tisa, kusudi hawa mitume na wanafunzi wa makanisa haya usiku wa leo, waweze kuondoka hapa wakiwa na ushuhuda wa namna ile ile, wangeweza kusema kesho, “Tunajua ya kwamba Bwana wetu amefufuka katika wafu Naye alituokoa na dhambi, alitupa Roho Mtakatifu. Alitumia midomo yetu kunena maneno ambayo sisi hatuninii, hata hatujui tunayozungumzia. Tulimwona akinena kupitia ndugu yetu, katika Roho wa unabii, kuleta ishara ya mwisho iliyoahidiwa Kanisa.”

¹⁷⁴ Tunaamini sasa, Bwana. Tusaidie sasa kukunja mikono yetu ya shati, kama vile tungalisema, utusaidie kuchimba ndani yake, jalia kila Mkristo katika kila ujirani. Tujalie, Bwana.

¹⁷⁵ Jalia kila mgonjwa aliye hapa, kila roho ya ibilisi ambayo imewashika hawa Wakristo, Wakristo hawa na wawe katika umoja na moyo mmoja, mpaka hapatakuwapo na mtu mnyonge miongoni mwetu usiku wa leo, ibada itakapomalizika. Tujalie, Bwana. Jionyeshe Mwenyewe hai usiku wa leo, Bwana. Ninapoondoka kwenye mji huu, Roho Wako hataondoka, atakaa hapa mpaka atakapourudisha mwili wa Bwana wetu Yesu.

¹⁷⁶ Wabariki ndugu zangu, Bwana. Wabariki dada zangu na hawa vijana wanaume na wanawake kwenye njia panda za maisha, jalia wafanye uamuzi wao usiku wa leo, kukutumikia Wewe. Tujalie.

177 Jalia watu wote wagonjwa watambue na kujua kutoka moyoni mwao ya kwamba Maandiko yameitabiri saa hii, na saa hii imewadia huku Grande Prairie, ambapo sisi, kama wahudumu Wako sote tunakubaliana ya kwamba tuko katika siku za mwisho na mambo haya yanapaswa kuweko.

178 Sasa, Baba, hivi hutakuja jukwaani kwa dakika chache na kuthibitisha ya kwamba Wewe upo hapa? Nimetoa ushuhuda Wako, sasa, Bwana, Wewe njoo ushuhudie ya kwamba nimesema kweli nasi tutakuamini Wewe, Bwana, kwa moyo wetu wote. Na kila mtu humu ndani ataponywa, ataokolewa kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

179 Nilimwambia mwanangu ningemaliza usiku wa leo saa tatu na nusu na ni saa nne kasoro dakika kumi sasa. Ninyi ni...Ninazungumza tu kwa muda mrefu sana. Yuko wapi? Nilisahau...Ndugu Fred, hivi—hivi walisambaza ninii za maombi...? Je, mlizitumia kadi hizi za maombi? Nilimwambia, ashuke aje, asambaze kadi za maombi. Sikujua kama walifanya hivyo au la, nami nilikuwa katika maombi waliponijia usiku wa leo, na—nami sikuwazia kuwauliza. Lakini alisambaza kadi ya maombi... Ni ngapi—ni ngapi zilizosambazwa? Ati nini? Ni ngapi na herufi zipi? Zilikuwa ni zipi, ulizosambaza kwanza? Kwanza, A, kwanza. Tulianza wapi hivi majuzi usiku? Moja?

180 Vema, hebu na tuchukue kadhaa za B. Tuchukue tu chache hapa juu. Tutamwombea kila mmoja wao. Hebu tuanzie kwenye B sasa, maana zile, labda, walikuwa hapa wapate kuziona hapo awali, za B ndizo mpya. Waliingia wangapi mstarini usiku huo? Kumi na watatu. Kumi na wanne. Vema, hebu na tuchukue kumi na tano kutoka kwa B, usiku wa leo.

181 Hebu tuone, hebu tuanzie, basi, hebu tuone, themanini na tano, themanini na tano, tisini, tisini na tano, mia moja. Hebu tuanzie kutoka themanini na tano. Ni nani aliye na kadi ya maombi B, themanini na tano? Inua mkono wako. Mtu huko nyuma...sasa kuna mikono miwili hapa juu. B, themanini na tano. Hiyo ni yako, bwana? Njoo hapa. B, themanini na sita. Ni nani aliye na kadi ya maombi B, themanini na sita? Mama huyu hapa. Waweza kusimama papa hapa? Themanini na saba, B, themanini na saba. Waweza kuinua mkono wako, tafadhali? Ili tujue wewe ni nani. Themanini na saba. Wasemaje? Themanini na tano. Hii ni themanini na sita, hapa, nafikiri. Themanini na saba, Hiyo ni tisini. Themanini na sita, kadi ya maombi B, themanini na sita. Una... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

182 Angetenda kama alivyotenda wakati huo, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule. Hiyo si ni kweli? Sasa aminini, kila mmoja wenu sasa. Iweni na kicho kabisa. Msisogeosogee huku na huku, aminini tu.

183 Sasa, loo, ndugu, sasa sikilizeni hili, ndugu...?... Hili ndilo. Sasa kama mtu yeyote ana shaka kwamba huyu si Mungu, basi

njoo hapa na uchukue mahali pangu. Njoo hapa ushuke kwenye mstari huu wa maombi. Acha Roho Mtakatifu anene kupitia kwako. Ukiwa na njia bora zaidi ya kufanya jambo hilo, hebu nijue. Naam, bila shaka ningeshukuru.

¹⁸⁴ Sasa, kila mmoja wa watu hawa kwenye mstari huu wa maombi, ni juavyo mimi, sikujui wewe. Ninyi ni Wakanada huku juu, nami ninatoka huko Marekani. Na kama siwajui, kila mmoja wenu katika mstari huu wa maombi, inueni mikono yenu, endapo siwajui. Kila mmoja. Ni wangapi huko nje kwenye kusanyiko wanaojua ya kwamba siwajui? Inua mkono wako, sijui lolote kukuhusu. Kila mtu, kadiri niwezavyo kuona.

¹⁸⁵ Ninawajua binti wawili wa Ndugu Evans, walioketi papa *hapa*, kwenye kiti hiki *hapa*, na nje ya hayo, hao ndio tu ninaoweza kuona ninaowajua. Naam, hawa hapa Dada Evans na Ndugu na Dada Dauch, papa *hapa*, papa *hapa*. Naam, vema.

¹⁸⁶ Sasa iweni tu na kicho kabisa. Sasa, mmenisikia nikishuhudia kutoka kwenye Maandiko na kuchukua mkutano wa ushuhuda wa kimitume. Kwamba hao mitume wakishuhudia, na bila shaka mimi. . . hiyo ilikuwa ni mchezo wa kuigiza, lakini kila kitu hasa nilichosema kilikuwa ni cha Kimaandiko. Mnaamini hilo? Kwamba, kilikuwa cha Kimaandiko, kilichowekwa katika mfano wa mchezo wa kuigiza.

¹⁸⁷ Sasa, kama Yeye ni Mungu wa kihistoria tu, basi alikufa na yote yamekwisha. Nasi tunaweza-. . . Ninyi watu huku juu kaskazini, mnajua ya kwamba hamwezi, mtu hawezi kupata joto kwa moto wa kuchorwa. Kama mtu alikuwa anakufa kwa baridi nawe ukamchukua, ukamwonyesha picha kubwa mno ya moto mkubwa, mzuri, mwekundu uliowaka wakati mmoja, hawezi kupata joto kwa moto wa kuchorwa. Wala hatuwezi kuokolewa na Mungu wa kihistoria. Hatuwezi kuongeza furaha ya Moto wa Kipentekoste isipokuwa uwe ni Moto ule ule leo hii. Hatuwezi—hatuwezi kumtumikia Mungu wa kihistoria.

¹⁸⁸ Naye ana faida gani kwenu, Mungu wa. . . aliyekuwa ndani ya Kristo, ikiwa Yeye si Mungu yeye yule leo ambaye aliahidi kuwa? Hilo ni la Kimaandiko, ewe rafiki. Sasa, jitikise kidogo tu. Usiwe na mhemuko, lakini amka tu kwa sekunde moja, kwamba hiyo ni kweli.

¹⁸⁹ Basi sisi hapa, huku mikono yangu ikiwa mbele za Mungu, Biblia yangu hapa, kwamba hatufahamiani. Katika mstari huu wa maombi, simjui hata mmoja wao, sijawahi kuwaona maishani mwangu. Sababu pekee ya wao kusimama hapa, mtu fulani alishuka, huyo mvulana, naye alikuwa na lundo la kadi na kuzichanganya na kumpa mtu kadi ya maombi. Nasi tukashuka usiku wa leo, na kusema tu, “Vema, nitaita kuanzia kwa namba fulani.” Tunaita kuanzia kwa namba nyingine.

¹⁹⁰ Hata si lazima uwe na namba, hata haikulazimu kuwa na kadi ya maombi, keti tu hapo na kusema, “Mungu, ninaamini ya kwamba Biblia ni ya kweli, nami ninaamini ya kwamba Wewe ndiye Kuhani Mkuu, nami ninaamini tunaishi katika siku za mwisho. Wala mtu huyu hanijui, nami ni mgonjwa, hebu aniambie nina shida gani. Acha—acha—acha anene nami kama alivyomfanyia yule mwanamke,” uone kitakachotukia. Asipofanya hivyo, basi mimi ni—mimi ni laghai na Biblia inasema uongo, na hiyo haiwezekani kwa Biblia kusema uongo. Ningeweza kuwa laghai, bali haiwezekani kwa Biblia kusema uongo. Lakini kama Biblia ikiunga mkono yale niliyosema, basi mimi si laghai, Mimi ni shahidi wa kufufuka Kwake nawe unaweza kuwa vivyo hivyo.

¹⁹¹ Sasa, hili si ni tukufu? Tafuta kujua. Dini nyingine iko wapi ulimwenguni? Nendeni mkamlete Mbudha, Mwislamu, hebu tuone kama *yu* hai, bali Kristo wetu *yu* hai. Nendeni mkachukue kanuni za imani, mwone kama zitafanya kazi, hazifanyi kazi; hazitaleta wokovu, hazitaleta mambo ya kimbinguni. Kama Mungu Mwenyezi, kama Roho Mtakatifu angekuwa sasa hivi na kufunua jambo moja, jambo moja tu, huo ungekuwa ni mwujiza mkubwa kadiri uwezavyo kutukia. Kweli kabisa, kwa sababu ni wa kimbinguni.

¹⁹² Ni nani angeweza kuwazia hilo? Ni nani angeweza kujua jinsi ambavyo m—mtu. . . watu wawili wasiojuana, hawajawahi kukutana maishani, na hata hivyo Roho anashuka na kufunua mambo yale hasa wanayofanya, na kuwazia, na yale wamefanya, yale watakayofanya, wala hayatahindwa? Huyu hana budi kuwa ni Mungu. Haiwezi kuwa kitu kingine. Kwa hiyo, mnaona, ninaapa, na ninajua, nanyi mnajua, ya kwamba mwanadamu hawezi kufanya mambo hayo, inahitaji Mungu. Kwa hiyo kama Yeye akithibitisha wakati mmoja kwamba ni kweli, basi ninyi nyote mnapaswa kufurahi na kushangilia. Pia kumbukeni, ni kwa ajili yenu pia. Mtafanya hivyo? Mtamkubali huyu Yesu ambaye nimekuwa nikiwaambia habari zake, kama Mponyaji wenu, kama atafanya hivyo? Mungu na atujalie.

¹⁹³ Sasa, Baba wa Mbinguni, huu ndio umbali niwezao kwenda, Bwana. Ninaweza tu kusema yale Neno lisemayo, inahitaji Wewe kulitimiza Neno. Hawa hapa watumishi Wako, wahudumu, watu watauwa, kuna wanawake watauwa, watumishi, wameketi kila mahali, wagonjwa na wanaoteseka. Kama ungalikuwa umesimama hapa umevaa suti hii, uliyonipa Wewe, usingeweza kuwafanyia cha zaidi. Kama wakija na kusema, “Bwana, utaniponya?” Mbona, Wewe ungesema, “Mtoto Wangu, nilifanya hivyo miaka elfu moja mia tisa iliyopita nilipopigwa kwa ajili ya uponyaji wako. Unasadiki haya?” Wangesema, “Naam, Bwana, lakini ninajuaje kwamba ni Wewe?” Ndipo ungeonyesha ya kwamba Wewe ulikuwa ndiye Kristo. Ungeweza kuwaonyesha, kufanya jambo ambalo—ambalo lingewathibitishia ya kwamba

Wewe ulikuwa ndiye Kristo, si kwa makovu ya misumari mikononi Mwako, kwa sababu mtu yeyote angeweza kuiga hilo. Lakini mambo ya kimbinguni ni kuingia katika maisha ya mtu huyo na kujua kile wanachofanya na kile kilichowaleta hapa, ndipo tunajua ni Roho Wako, Wewe, Mzabibu mkuu, ukitenda kazi katika matawi Yako.

¹⁹⁴ Na iwe hivyo usiku wa leo, tena, Bwana. Liheshimu Neno Lako. Utusamehe dhambi zetu kama tulivyowasamehe waliotukosea. Tupe utamu wa roho na jalia Roho Mtakatifu sasa, aje upesi na kulithibitisha Neno, ili kila mtu hapa ndani apate kujua ya kwamba Mwana wa Mungu hajafa, bali amefufuka katika wafu na yu hai baada ya miaka elfu moja mia tisa, na yu hai milele na milele. Kwa Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹⁵ Sasa, wekeni tu usikivu wenu. Ombeni tu na . . . Vema. Huyo ndiye yule mtu? Vema. Sasa, ninawatakeni kila mmoja, kila mtu awe macho, awe macho. Na uwe ukiomba, ukisema, “Bwana, ninateseka na *hiki-na-hiki*. Hebu Ndugu Branham anigeukie tu, ninajua yeye hanijui, hajui nina shida gani, bali kama tu utasema naye, ninajua nimekugusa Wewe.” Sasa, ungeweza kunigusa usiku kucha na iwe kama ni kugusa dawati hilo, ingekuwa ni bure, unaona. Lakini mguse tu Yeye, wakati mmoja, uone kinachotukia, unaona. Imani yako ilingusa.

¹⁹⁶ Sasa, huyu hapa mtu ambaye ametokea kuwa . . . Kama ninaweza kumleta mtu fulani hapa mbele yangu kwanza, mnaona, maana baada ya kuzungumza, na kadhalika, basi . . . Ni—ninazungumza naye, kama tu vile Yesu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, mpaka akaona shida yake ilikuwa nini kisha akamwambia, naye akasema, “Mbona, hiyo ilikuwa ni kweli.” Basi mnaona, sasa hivyo ndivyo ilivyo na mtu huyu.

¹⁹⁷ Sasa, hatufahamiani, siuyo, bwana, mimi na wewe? Ninataka tu usogee moja kwa moja *hapa*, kusudi nikupate, kusudi tu niweze kuninii, nisuingalie mstari huo wa maombi. Wao wakiangalia huku, wananinii . . . wakati mwingine Roho huondoka na wengine wana imani kuu, ya hali ya juu, anawaendea.

¹⁹⁸ Ningependa kuzungumza nawe kwanza. Sasa, sisi ni watu wawili tofauti, watu wawili ambao tumekutana kwa mara yetu ya kwanza maishani. Hiyo ni kweli, siuyo? Vema. Sasa, kama kuna ninii . . . Sina fununu kuna shida gani, si—sijui. Basi kama mimi—kama ningeweza kukusaidia upate afya, ama huenda ukawa na matatizo ya kinyumbani, huenda ukawa na matatizo ya kifedha, huenda ukawa mgonjwa, huenda ukawa na kansa, huenda ukawa na uvimbe, huenda ukawa na TB, sijui, unaona, sina habari, lakini kama ningeweza kukusaidia halafu nisikusaidie, afadhali niondoke jukwaani, ningekuwa mnafiki, nisingestahili kusimama hapa nyuma. Lakini kama mimi . . .

Kama Yesu angekuwa amesimama hapa, nawe ungemwomba akusaidie, nawe. . . kwamba Yeye—Yeye angekujalia wewe. . .

¹⁹⁹ Sasa, ukitaka kujua ilikuwa ni Yeye. . . Mtu yeyote angeweza kuwa na makovu ya misumari mikononi mwake na misu- . . . alama kwenye paji la uso wake. Lakini roho fulani. . . Mnaona, kwa sababu kama angekuwa amesimama hapa, ule Utawala wa Miaka Elfu ungekuwa unaendelea. Yeye hatakuja tena duniani mpaka atakapokutana na Kanisa hewani. Tunanyakuliwa pamoja Naye kumlaki hewani, kisha anarudi pamoja na Kanisa Lake. Kwa hiyo asingeweza kuwa hapa duniani namna hiyo, ila tu ni Roho Wake katika Kanisa Lake.

²⁰⁰ Sasa, mnaamini. . . ? Sasa, Malaika wa Bwana aliniambia. . . Kama labda mmesoma kitabu changu, sijui. Lakini yeye. . . Mlikisoma, vema. Mnakumbuka huko kwenye kile kinu usiku ule, wakati alipozungumza nami na kusema, “Kama unaweza kuwafanya watu wakuamini, kisha uwe mwaminifu unapoomba, hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi yako?”

Nikasema, “Mimi, hawataniamini, si—si—sina elimu.”

²⁰¹ Akasema, “Kama vile Musa alivyopewa ishara mbili kwa ajili ya thibitisho, nawe vivyo hivyo.” Kasema, “Kwanza, utashika mikono ya watu, ndipo utajua kuna shida gani. Baada ya hayo, kama utakuwa mwaminifu, itakuwa ya kwamba utajua mawazo yenyewe ya mioyo yao.” Naye akasema, “Itawabidi kuamini jambo hili.”

²⁰² Ni wangapi wanaokumbuka hayo yakitabiriwa nilipokuwa hapa mara ya kwanza, ama, miaka mingi iliyopita, na kuwaambia ititimia? Sasa, angalieni kama ilitimia au la. Niangalieni tu, kama vile Yohana, Petro na Yohana walipopitia langoni, yule mtu aliyekuwa kiwete, kasema, “Tutazame sisi.” Nao wakamwangualia. Kitu gani? Alikuwa akijaribu kuvutia usikivu wake.

²⁰³ Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.” Mnaona? Wewe ni roho ndani ya mwili huo, hiyo ndiyo ninayoshughulikia, kuna roho *hapa* ndani. Sasa, sikujui kwa roho yangu, wala wewe hunijui, bali Mungu anatumia sote wawili. Kwa hiyo basi, itabidi kuwepo na Kitu fulani ndani yangu kukwambia, ndipo utajua kama ni kweli ama si kweli. Kama ni kweli, vema basi, inatoka kwa Mungu; kama si kweli, si Mungu. Hilo ni jambo la kimantiki, sivyo?

²⁰⁴ Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, huyo ni mwanamke. Ni mke wako, naye hayupo hapa. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake? Ungeamini basi? Amekuwa na kiharusi. Hiyo ni kweli. Unaamini atakuwa mzima sasa, roho hiyo iliyo juu yako? Utakapomwendea, weka mikono yako juu yake, katika Jina la Bwana Yesu, usiwe na shaka, kitamwacha. Nenda sasa na uamini. Mungu akubariki.

205 Unaamini? Unaamini? Mwulize huyo mwanamume kama mambo hayo yalikuwa ni kweli. Iweni tu na imani sasa, iweni na kicho kabisa. [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Mradi tu ninaweza kusimama.)

206 Hatufahamiani. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Wewe ni mdogo wa umri kuliko mimi. Ka—kamwe sijawahi kukuona. Lakini labda mwanamke yule aliyekutana na Bwana wetu kisimani wakati huo, labda alikuwa na umri mdogo kuliko Yeye alivyokuwa, na hiyo ilikuwa mara yao ya kwanza kukutana. Nasi hapa tunakutana kama tu walivyokutana.

207 Sasa, wewe ni mwanadamu, mimi ni mwanadamu. Sikujui, hunijui mimi, lakini kwa kuwa Wakristo, basi tuna Baba anayetujua sote wawili. Kama anaweza kuniambia jambo fulani lililokuleta hapa, ama jambo fulani ambalo umefanya, jambo ambalo hukupaswa kufanya, kama Yeye anaweza kukwambia yale yamekuwako, hakika unaweza kuamini yale anayosema yatakuja ni ya kweli, kama akikwambia yale yamekuwako.

208 Sasa, kama nikija hapa na kusema, “Mungu alinipa karama ya uponyaji.” Ninaweza mikono yangu juu yako, “Utukufu kwa Mungu! Ponywa,” ungeweza kuamini hilo, hilo lingeweza kuwa ni kweli, na hiyo ni kweli. Ninaamini hilo kwa ninii yote. . . Biblia ilisema hivyo. Lakini sasa, hebu twende mbele zaidi ya hapo, tumekuwa na siku hiyo, hebu twende mbele kupita hayo.

209 Na sasa, vipi kama Yeye akisimama hapa sasa na anaweza kukwambia kile ulicho, kile unachotaka, na shauku za moyo wako, na siri ya moyo wako, na mambo maishani mwako unayohitaji, au ambayo hukupaswa kufanya? Kama hayako chini ya Damu basi Yeye atayafichua, unaona. Sasa, kwa sababu kama yako chini ya Damu, yako katika Bahari ya Usahaulifu, hakuna mtu anayeweza kuyachimbua hayo. Hiyo ni kweli.

210 Wewe ni Mkristo. Mtetemo wa roho yako, hivyo ndivyo ninavyouita, ninajua wimbi hilo, unajisikia kukaribishwa, unaniamini. Mimi. . . Wewe fanya hivyo. Unaona? Mara ulipokuja, nilijua hilo. Ungeweza kuwa m—mdanganyifu, ukaja hapa, na basi nini kingetukia? Mmesikia yaliyowapata, wengi wamelala wamepooza usiku wa leo, wengi kaburini kwa ajili ya jambo hilo. Hatuigizi kanisa, tunamtumikia Mungu.

211 Una wasiwasi sana, una ninii. . . ulikuwa na mengi niani mwako, maisha magumu, maisha yako ya nyuma, wasiwasi mwingi na shida. Pia unaugua henia, hiyo ni kweli. Sasa, je, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Naam, unaamini.

212 Na unafikiri hiyo ilikuwa ni kubahatisha? Ngoja kidogo, ngoja kidogo, ana mawasiliano mazuri sana na Mungu, maskini mama huyu.

213 Sijui nilichokwambia, lakini chochote kile, kilikuwa ni kweli. Hiyo ni kweli? Sasa, kama itatubidi kusimama na

mwanamke huyu sasa hivi, kwa kuwa anaweza kuzungumza na mtu fulani, roho mzuri sana. . . Hata hivyo, wasiwasi, hiyo ni kweli, na ugonjwa wa fadhaa, naye Shetani anakusumbua juu ya jambo hilo, anasema utarukwa na akili na kila kitu, bali wewe ni. . . anadanganya.

²¹⁴ Ulikuwa na henia, naona hilo, ukingojea upasuaji, lakini huo. . . Una, pia, mishipa iliyovimba kwenye viungo vyako. Hiyo ni kweli. Halafu una mtu fulani moyoni mwako, mtu huyo yupo hapa, mume wako. Unafikiri kama Mungu anaweza kuniambia tatizo la mume wako, utaamini? Ni mgongo wake. Hiyo ni kweli. Hili hapa jambo lingine, ninamwona mtoto akitokea. Unaomba na kumjali mtoto, mtoto huyo ana shida fulani, ni kwa sababu hasomi vizuri sana. Hiyo ni kweli. BWANA ASEMA HIVI. Mambo hayo ni kweli? Je, unayakubali yote kama tiketi ya ukombozi kutoka kwa Mungu kwa ajili yako? Nenda, na itakuwa tu jinsi ulivyoamini. Mungu awe pamoja nawe.

Unaamini? Amini, amini.

²¹⁵ Sikujui wewe, hatufahamiani. Mama? Umekutana nami hapo awali. Unanifahamu, mimi sikujui. Mnaona, watu wengi wananjua, wanakuja tu mikutanoni na mahali mbalimbali namna hiyo, lakini sijui kamwe, sijui chochote kukuhusu. Unaona? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Ninaamini hilo. Una henia, hiyo ndiyo shida yako. Wala hutoki kwenye mji huu, bali Alberta, mahali panapoitwa Easton. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Hilo lingekusaidia? Bibi Braun. Sasa, nenda ukaponywe. Unaweza kupata ulichoomba. Mungu akubariki.

Unaamini? Unaamini?

²¹⁶ Unaamini Mungu anaweza kunifunulia shida yako ni nini? Uko hali mbaya. Unakabiliwa na upasuaji, ndivyo daktari alivyosema, kidogo ni mtu mwenye nguvu. Ni tatizo la kike. Nawe huamini katika upasuaji, hiyo ndiyo sababu umekuja kwangu nikuombe. Nawe ulijisikia moyoni mwako ulipoomba, kama ungeweza kufika hapa jukwaani, niweke mikono yangu juu yako, hungehitaji huo upasuaji. Kama hilo ndilo ombi lako, inua mkono wako, Dada. Ninajuaje ulichomwomba Mungu? Njoo hapa.

Katika Jina la Yesu Kristo, shauku yake na itimizwe. Amina.

Usiwe na shaka, amini.

²¹⁷ Sasa, hatufahamiani. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Unafikiri bega lako litakuwa sawa? Uligusa nini? Litakuwa sawa sasa. Niliona mwanamke mkubwa zaidi akitokea hapa, ulikuwa ukiomba. Vema. Imani yako inakuokoa sasa.

Aligusa nini?

218 Maskini mama huyo aliyeketi hapo aliyevaa kofia nyeusi akiniangalia, naam, wewe, ugonjwa wako wa tumbo umekuacha sasa. Nenda, ukale chakula chako cha jioni. Yesu Kristo anakuponya. Wote umekwisha sasa, nenda ukale. Ulikuwa na ugonjwa wa kidonda tumboni mwako, yote yamekwisha.

219 Vipi kuhusu hayo maumivu ya kichwa, msichana, uliyeketi hapo nyuma? Unaamini Mungu anaweza kuponya maumivu ya kichwa na kukupa afya? Naam. Ulikuwa na imani zaidi ya ulivyodhani ulikuwa nayo, sivyo? Maumivu yako ya kichwa yatakoma sasa. Kwa kweli, hunayo sasa.

Aligusa nini? Hebu wazieni tu, aligusa nini? Alimgusa Kuhani Mkuu.

220 Huyu mama aliyeketi huko nyuma kabisa mwenye yabisi kavu huko, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, huko nyuma? Huyu mwanamke aliyevaa miwani, sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu, bali umeketi huko nyuma ukiomba. Kama ndivyo ilivyo, simama kwa miguu yako. Mungu akubariki. Kamwe hutalemazwa nayo.

221 Ninakupa changamoto kumwamini Yeye. Siwajui watu hawa, sijawahi kuwaona. Lakini Bwana wangu anawajua.

222 Huyu mtu anayeketi yapata wa pili nyuma kutoka mwisho huko nyuma, akiagua ugonjwa wa tumbo, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unaukubali? Mungu akubariki. Una kadi ya maombi? Una kadi ya maombi? Unayo? Hutaihitaji.

Mungu anaweza kuponya kisukari, sivyo? Vema. Nenda, ukiamini, amini tu.

Yeye huponya wasiwasi, pia, hivi huamini hilo? Endelea kutembea, ukisema, "Asante, Bwana." Amini tu kwa moyo wako wote.

Njoo. Yeye huponya yabisi kavu, unaamini hilo? Basi endelea tu kusonga mbele. Naam, bwana.

223 Hebu kidogo, jambo fulani lilitukia. Njoo hapa. Bila shaka tunaona unatembea kwa fimbo, sitataja hilo. Lakini kisukari chako na ugonjwa wa moyo, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unafikiri Yeye atakuponya? Unaamini? Mungu atakuponya? Endelea kusonga mbele, ukisema, "Asante, Bwana." Endelea, uwe mzima. Sema, "Asante, Bwana."

Mnaamini, kila mtu? Aminini tu, msiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote.

224 Vipi kuhusu ugonjwa huo wa kibofu nyongo, uliyeketi hapo ukutani? Unaonekana mwaminifu sana. Sikujui, sivyo? Hatufahamiani, mmoja kwa mwingine. Lakini hiyo ndiyo shida yako. Hiyo ni kweli, sivyo? Hivi hatufahamiani, sisi kwa sisi? Inua mkono wako. Shida yako ilikuwa hiyo? Vema, bwana. Ulikuwa umeketi pale ukiomba, ukitaka Mungu akuguse. Ulimgusa Naye akanigusa. Sasa, Clarence, Bw. Rouin, unaweza

kwenda nyumbani, uwe mzima. Mungu anakuponya. Hilo ndilo jina lako, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

225 Sijawahi kumwona. Unaamini? Ni wangapi wenu mnaoamini kwa moyo wenu wote? Mbona, ni Kristo hapa, marafiki. Ninataka kuwaonyesha jambo fulani. Ndugu zangu hapa ni watu wa Mungu. Wana haki ya kuwaombea wagonjwa kadiri nilivyo nayo mimi. Njoni hapa, ndugu, njoni hapa. Jiwekeni tu kila upande, na mfanye mistari miwili, moja kwa moja hapa. Ninawatakeni mwone nitakapoondoka, haiwabidi kuningojea nirudi. Hawa hapa watu wa Mungu, huwaombea wagonjwa pia.

226 Fanyeni tu mistari miwili papa hapa sasa, njoni moja kwa moja pande zangu zote mbili. Sitaki kuliacha kusanyiko likifikiri kwamba mwinjilisti fulani hana budi kuja na kuwaombea wagonjwa. Ninataka kuwaonyesha ya kwamba Mungu atawaponya wagonjwa kupitia maombi ya wanaume hawa.

227 Ni wangapi hapa walio na kadi za maombi? Inueni mikono yenu. Kwa namna fulani chukueni namba zenu. Za A zote kwanza, pangeni mstari papa hapa. La, ngojeni. Wapi, ninii tu, tuliachia wapi? Sawa, mimi... Vema, hebu—hebu... kabla hatujafikia... Hebu kidogo, msipofanya hivyo, tutachanganyikiwa kabisa. Hebu watu hawa hapa walio na kadi ya maombi A, waingie mstarini. Kwamba... A na B waingie mstarini hapa, hii, sehemu hii hapa, fanyeni mstari papa hapa, A na B. Kwenye sehemu hiyo tu sasa. Hebu kidogo. Chukueni tu, chukueni upande ule pale. Tutamfikia kila mmoja. Hebu kidogo. Hebu kidogo sasa, mpaka tutakapomfikia kila mmoja, mnaona. Tuta—tutamfikia kila mmoja.

228 Wote upande huu wenye A na B, jipangeni. Sasa, itatubidi kuwarudisha hawa hapa nyuma upande ule mwingine tutakapowafikia, mnaona. Hatuna budi kushughulikia upande mmoja kwa wakati mmoja. Wote walio na A na B, pangeni mstari upande huu. Vema. Sasa, mara upande huu utakapopita, acheni safu hii ya katikati ipitie upande ule, wakiisha kushughulikiwa. Na mara tu watakaposhughulikiwa, acheni upande huu upite. Kila mtu atakayeamini na kupitia hapa, akimwamini Mungu kabisa... .

229 Mnaogopa? “Msiogope, ni mimi,” alisema Bwana Yesu. Hivi hamwamini ni Yeye? Ni wangapi wanaoamini ni Yeye? Sasa angalieni, ikiwa Yeye yuko hapa... Kwa sababu tu Yeye alinifanya mwonaji, aliwafanya wanaume hawa wahudumu, mnaona, wana Roho yule yule niliye naye, Mungu yeye yule, Roho Mtakatifu yeye yule, agizo lile lile mbele za Mungu, kuwaombea wagonjwa, mikono ile ile, Roho yeye yule, wametiwa mafuta, wanaweza kufanya hivyo, sawa na mimi. Tutasimama hapa pamoja na kumwombea kila mmoja

wenu, mnapopitia hapa, tukiweka mikono yetu juu yenu. Na unapopitia hapa, tenda kama kwamba umeponywa. Upitie hapa ukisema, “Asante, Bwana.” Kisha urudi huko nje na kuangalia tatizo lako la tumbo na mambo haya mengine yote yakikuacha. Unaamini hilo?

Na tuombe sasa pamoja tunapoinamisha vichwa vyetu.

²³⁰ Bwana Yesu, Wewe upo hapa, ulijithibitisha Mwenyewe hapa, Bwana, kila mahali jengoni, ukiwaambia watu, ukiwaita. Na hawa hapa watumishi Wako wamesimama, Bwana. Nami ninataka watu hawa hapa wajue ya kwamba watumishi Wako, si lazima wangojee mtu maalum apitie huku, mwinjilisti fulani maalum, lakini Mungu, wanaweza kwenda moja kwa moja, wamwite mchungaji wao, hao ni watumishi Wako, nao hawa hapa ninapowaita, kama askari halisi waliosimama moja kwa moja mbele ya kusanyiko. Wao ni waaminio, wako tayari, wametiwa mafuta kuweka mikono yao juu ya wagonjwa.

²³¹ Na Mungu Mwenyezi, aliyemfufua Yesu, ambaye ni Mwokozi wetu, anayesimama katikati yetu usiku wa leo, tutie mafuta, Bwana, ututie mafuta kwa Roho Wako Mtakatifu, ili kwamba tunapoweka mikono juu ya watu hawa, jalia baraka za Mungu zije juu yao, na jalia kila mmoja wao aponywe. Tujalie, Bwana. Tunawaanzisha kupitia hapa, na kuwaombea, katika Jina la Yesu Kristo.

²³² Basi Shetani, tuna neno kwa ajili yako: Tunataka kukwambia ya kwamba umewadanganya watu mradi tu utafanya hivyo. Huna haki ya kisheria kuwashikilia. Yesu Kristo alichukua kila haki uliyokuwa nayo wakati alipofufuka katika wafu. Yeye alikushinda, nawe si kitu ila mdanganyifu, Naye yupo hapa usiku wa leo kuonyesha ulaghai wako, na kukufichua, na kukwambia wewe ni nani. Wala huwezi kushikilia kusanyiko hili tena. Tunachukua kusanyiko hili, watu hawa wagonjwa hapa, watoto wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, kukutupilia mbali kutoka kwao, nawe itakubidi kuwaacha. Tutaweka mikono yetu juu yao kulitimiza Neno la Mungu. Watakapopitia hapa, mioyo yao itajaa utukufu wa Mungu nao wataondoka hapa wakimsifu Mungu. Wataponywa, na kutakuwa na uamsho.

Ee Mungu, tujalie, katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo, kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

²³³ Sasa, kama kusanyiko, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kama hamwezi kuomba, imbeni, huku mtu fulani akiongoza uimbaji.

Amini tu, tu. . .

Sasa, kila mmoja, unapopita, amini sasa unapopita.

[Ndugu Branham anawaombea watu, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.] . . . ? . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.]

Nampenda, nampenda,
kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²³⁴ Loo, jinsi ninavyompenda Yesu! Hivi hammpendi? Yeye si ni wa ajabu? Usininii. . . Loo, hii kwangu ni kama Mbinguni. Unaweza. . .? Loo, sina mhemko, la, sidhani, wa kupita kiasi. Lakini ninahisi tu hisia tamu sana, kama tu vile Baba wa Mbinguni angesema, “Ulifanya vema.”

²³⁵ Kila mtu aliombewa? Ni wangapi wanaoamini utakuwa mzima sasa? Inua mkono wako. Kila mmoja. Angalieni, Roho wa Mungu akipitia mkutanoni, akija moja kwa moja, hivyo ndivyo alivyosema hasa. Kuna jambo moja tu la kuzuia, kama tu huamini, halitatukia; kama unaamini, haina budi kutukia, tayari imekwisha. Mnaona? Ni kazi iliyomalizika. Loo, Yeye si ni wa ajabu? Loo, ninampenda tu.

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari. . . (Amemaliza? Nini. . .? . . .)

[Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.]

. . . Nampenda,
Kwani. . .
. . . kununua (. . .? . . .) . . . wokovu
Juu ya. . .

Hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu kwa dakika moja.

²³⁶ Baba wa Mbinguni, najua hapo kwenye kusanyiko ameketi mtu ambaye, Shetani amemfunga, naye anajaribu kumshikilia huyo mwanamke. Mungu, jalia kwamba atamwacha. Mtu mzuri, kwa nini asiwe huru? Ninaomba ya kwamba utatujalia, Baba. Kwa njia ya Yesu, Mwanao, tunaomba. Amina.

Na. . . napenda. . .
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari. . .

²³⁷ Je, kuna mwenye dhambi hapa, angetaka kumkubali Kristo kama Mwokozi wao? Katika Uwepo wa Mungu sasa, angesimama tu, aseme, “Ninamkubali kama Mwokozi wangu”? Je, huenda kuna mtu hapa ambaye amerudi nyuma, na angetaka kumrudia Mungu, sasa hivi, chini ya upako wa Roho Mtakatifu?

²³⁸ Mungu akubariki, mwanangu. Mungu na akujalie. Katika Jina la Yesu Kristo, ninakupa shauku ya moyo wako. Rudi sasa kwenye Nyumba ya Mungu, ukiliitia Jina Lake, ukaishi mwaminifu Kwake.

²³⁹ Mchungaji, hakika ninathamini ushirika huu mzuri. Kwa nini hukuuliza? Hmm! Huyu ni mchungaji, acha kusanyiko

lake lipite, na asijiombea mwenyewe. Damu hiyo itakoma. Ubarikiwe, Ndugu.

²⁴⁰ Ndio kwanza nishike mkono wake hapa na mtetemo ukienda mbio, ungeweza ukawa kansa. Atakuwa mzima sasa. Hakuniambia neno juu yake, hakulitaja kamwe. Nililishika tu wakati alipoushika mkono wangu.

Mungu akubariki, Mchungaji. Mungu awabariki, kusanyiko.

Hata tutakapokutana! hata tutakapokutana!

Hata tutakapokutana pa Yesu... (Mungu awabariki kila mmoja wenu, ndugu zangu.

Mungu awabariki, ndugu.)

Mpaka... (Mungu akubariki, Ndugu...?..)

Hata tutakapokutana! (Mungu, pa Yesu...?..)


Mungu awe nanyi hata tutakapokutana tena!

Ninapowapa mchungaji wenu, hebu na tuinamishe vichwa vyetu na tuuimbe kwa utulivu.

Hata tutakapokutana!

²⁴¹ Mungu wa Mbinguni na awe pamoja nanyi daima, awaneemeshe daima. Nitakuwa nikiwaombea. Niombeeni hata tutakapokutana. Kukutana wapi?

...miguuni pa Yesu; (Hata tutakapokutana!)

²⁴² Mungu akubariki, Mchungaji. Mungu akubariki...?.. 

61-0517 Ni Mimi
Zion Gospel Tabernacle
Grande Prairie, Alberta Canada

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org